# Violation of cooperative principles among Facebookers in a Kenyan political discourse

*Research Article*

Published in Nairobi, Kenya by Royallite Global in the ***Research Journal in African Languages***, Volume 2, Issue 3, 2021

© 2021 The Author(s). This article is distributed under a Creative Commons Attribution (CC-BY-NC-SA) license.

**Article Information**
Submitted: 15th August 2021
Accepted: 28th November 2021
Published: 10th December 2021

Additional information is available at the end of the article

https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/

*To read the paper online, please scan this QR code*

**Walter Akello Odiaga [1], Riro Matinde[2] & Stephen Oluoch [3]**
Department of Languages, Linguistics and Literature, Kisii University, Kenya
Correspondence: walterodiaga@gmail.com
https://orcid.org/0000-0003-0346-2123

**Abstract**
This study investigated Cooperative Principles that are violated by facebookers while discussing political issues in Kenya. The research was guided by the theory of Cooperative Principles of Grice (1975) that advocates for the adherence of certain conversation maxims in a conversation. The study adopted a qualitative research design since it intended to explain a naturally occurring phenomenon. The study used the Facebook pages of Rt. Hon. Raila Odinga and Hon. William Ruto as sources of data. The study adopted purposive sampling to identify eighty-five comments to form data. The eligibility criterion for choosing the sample included comments posted between 1st January to 30th April 2021. In collecting data, the researcher recorded the comments made by the participants from the Facebook pages. To enhance validity of data, the researcher used newspaper cuttings from the local dailies. Using the tenets of the theory, the researcher used content analysis to analyze his data. The study showed that facebookers violate all the cooperative principles while discussing political issues in Kenya. The study concluded that there is need for interlocutors to engage cooperative principles in there discourse so as to bring satisfactory meaning out of their comments.

**Keywords:** cooperative principles, Facebook, political discourse

**How to Cite:**
Akello, W. O., Matinde, R., & Oluoch, S. (2021). Violation of cooperative principles among Facebookers in a Kenyan political discourse. *Research Journal in African Languages*, 2(3). Retrieved from https://royalliteglobal.com/african-languages/article/view/703

# Ukiukaji wa Kanuni za Ushirikiano miongoni mwa washiriki wa mtandao wa *Facebook* katika diskosi ya siasa nchini Kenya

Published in Nairobi, Kenya by Royallite Global in the ***Research Journal in African Languages***, Volume 2, Issue 3, 2021

© 2021 The Author(s). This article is distributed under a Creative Commons Attribution (CC-BY-NC-SA) license.

**Article Information**
Submitted: 15th August 2021
Accepted: 28th November 2021
Published: 10th December 2021

Additional information is available at the end of the article

https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/

*To read the paper online, please scan this QR code*

**Akello Odiaga Walter[1], Riro Matinde[2] & Oluoch Stephen[3]**
Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi, Chuo Kikuu cha Kisii, Kenya
Barua pepe: walterodiaga@gmail.com
https://orcid.org/0000-0003-0346-2123

**Ikisiri**
Utafiti huu ulichunguza kanuni za ushirikiano zinazokiukwa na washiriki wa mtandao wa Facebook wanapojadili masuala ya kisiasa nchini Kenya. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Kanuni za Ushirikiano ya Grice (1975) inayojihusisha na kanuni mbalimbali zinazofaa kuongoza mchakato wa mazungumzo. Utafiti huu ni wa kistahilifu na mtafiti alitumia kurasa za Facebook za wanasiasa Raila Odinga na William Ruto kama vyanzo vya data. Mtafiti alitumia sampuli kusudio kuteua kauli themanini na tano kama data za utafiti. Mtafiti alikusanya kauli zilizowekwa na washiriki kati ya Januari 1 hadi Aprili 30, 2021. Kipindi hiki kilishuhudia matukio mengi ya kisiasa, hivyo kilikuwa muhimu kwa utafiti huu. Mtafiti alitumia mbinu ya kunakili ili kudondoa data kutoka kwa kurasa hizo. Mtafiti pia alikusanya data kwa kuyadurusa machapisho kama vile magazeti ili kuhalalisha data zake. Kupitia kwa mihimili ya nadharia ya utafiti, data za utafiti zilichanganuliwa kwa kutoa maelezo. Utafiti ulibainisha kuwa kanuni zote za ushirikiano hukiukwa na washiriki wa mtandao wa Facebook wanapojadili masuala ya kisiasa nchini Kenya. Utafiti huu ulihitimisha kuwa kuna haja ya washiriki katika mchakato wa mawasiliano kuhusisha kanuni za ushirikiano katika mazungumzo yao ili kufanya jumbe zao kuwa timilifu, hivyo, kueleweka vizuri.

**Maneno Muhimu:** kanuni za ushirikiano, diskosi ya siasa, *Facebook*

**How to Cite:**
Akello, W. O., Matinde, R., & Oluoch, S. (2021). Violation of cooperative principles among Facebookers in a Kenyan political discourse. *Research Journal in African Languages*, 2(3). Retrieved from https://royalliteglobal.com/african-languages/article/view/703

Crossref Cited-by

**Public Interest Statement**

Political conversations usually involve use of persuasive statements that are meant to sway one to join forces with another. This discourse equally involves statements that depict those considered not to be allies of an individual as unfit and hence not suitable to hold any public office. Being a discourse of persuasion and mudslinging, interlocutors usually find themselves producing statements that are not precise, untrue, distorted and out of context. This study demonstrates that interlocutors who use Facebook to discuss political issues in Kenya often violate the cooperative principles, thus making their statements to have the ability to threaten face.

**Utangulizi**

**1.0 Usuli wa mada**

Katika mazungumzo yoyote, msikilizaji anatakiwa kuelewa ujumbe na kusudi la uneni uliotolewa na mzungumzaji, mbali na kutakiwa kuweza kutoa mwitiko ambao unaoana na kauli iliyotolewa. Kwa kufanya hivyo, washiriki katika mchakato wa mazungumzo hujipata katika mchakato wa mazungumzo timilifu. Matumizi ya mitandao ya kijamii kama vile *Facebook* na *Twitter* huwapa wanajamii jukwaa muhimu la kuwasiliana na wengine bila udhabiti wowote. Kutokana na uhuru uliopo wa kimawasiliano katika mitandao hii, washiriki hujipata wakitumia lugha isiyo rasmi ambayo huwalazimu wapokezi wa jumbe zao kutumia vimanilizi vya mazungumzo ili kufasiri maana kutoka kwazo. Hata hivyo, ufasiri usiofaa wakati mwingine huchangia kutolewa kwa miitiko isiyofaa, hali ambayo husababisha kutokea kwa kutoelewana kwa wahusika. Hali hii ikitokea, nyuso za wahusika hukiukwa. Ili kuzuia hali hii, washiriki wanalazimika kufuata na kuzingatia kanuni za ushirikiano za Grice (1975) ambazo huongoza mchakato wa mazungumzo. Hata hivyo, kutokana na kuwepo kwa uhuru wa kimawasiliano katika mitandao ya kijamii kama vile *Facebook*, aghalabu kuna baadhi ya washiriki ambao hukosa kufuata kanuni hizi, hivyo, kuzikiuka. Makala hii basi ilinuia kuchunguza aina za kanuni za ushirikiano zinazokiukwa na washiriki wa mtandao wa *Facebook* katika diskosi ya siasa nchini Kenya. Utafiti huu ni muhimu kwani utachangia katika kuendeleza zaidi taaluma ya pragmatiki.

**2.0 Suala la utafiti**

Siasa ni mojawapo ya masuala tata katika jamii ambalo limeweza kutafitiwa na watafiti mbalimbali walioweza kuchunguza lugha ya siasa katika msingi wa mwingiliano kati ya siasa, lugha na jamii. Lugha ni chombo muhimu katika asasi za siasa na utawala. Lugha huweza kutumika na wanajamii kuunganisha au kutenganisha jamii kisiasa. Hivyo basi, lugha huathiri mtagusano kati ya siasa na jamii. Michango ya siasa katika jamii ni sababu kuu ambayo inaufanya utafiti wake kuwa na msingi. Michango hii inadidimizwa na kukosekana kwa mawasiliano timilifu ambayo huzuka kwa sababu ya kukiukwa kwa kanuni za ushirikiano, hali ambayo huchangia kuwepo kwa vitendo vinavyoathiri nyuso za wahusika. Mapitio ya maandishi yaliyodurusiwa yalidhihirisha kuwa tafiti chache sana zimeshughulikia suala la ukiukaji wa kanuni za ushirikiano katika diskosi ya siasa hususan katika muktadha wa Kenya. Tafiti nyingi zilizoendelezwa kuhusu suala hili zimefanywa katika nchi za magharibi. Hili ni pengo la utafiti ambalo lilifaa kuzibwa.

**2.1 Lengo la utafiti**
Kuchunguza kanuni za ushirikiano zinazokiukwa na washiriki wa mtandao wa *Facebook* wanapojjadili masuala ya kisiasa nchini Kenya.

**2.2 Swali la utafiti**
Je, ni kanuni zipi za ushirikiano hukiukwa na washiriki wa mtandao wa *Facebook* wanapojadili masuala ya kisiasa nchini Kenya?

**3.0 Uhakiki wa Maandishi**
**3.1 Mawasiliano ya Kimtandao**
Kulingana na Locher (2010), mawasiliano ya kimtandao ni mawasiliano yanayofanyika kupitia zana za kielektroniki. Haya ni mawasiliano yanayofanyika kati ya wanadamu kupitia mfumo wa kompyuta. Miaka 20 iliyopita, mfumo huu wa mawasiliano haukutumika nje ya taasisi za kiakademia kule Marekani. Hata hivyo, leo hii, mfumo huu wa mawasiliano unatumika na mamilioni ya watu kote duniani. Wanaoshiriki katika mawasiliano ya kimtandao wanaweza kuendeleza mawasiliano yao pasi na kujitambulisha kwa utambulisho wao wa kweli.

Kiesler na wenzake (1984) wanaeleza kuwa kukosekana kwa utambulisho wa kweli katika mawasiliano ya kimtandao kumesababisha kuwepo kwa uhuru wa kujieleza jambo linalosababisha kutokea kwa uhasama na ukiukaji wa hisia za washiriki. Kulingana nao, katika mawasiliano haya, mshiriki anatathminiwa kwa kuzingatia anachosema. Kulingana na Hiltz na Turoff (1993) washiriki katika mawasiliano ya kimtandao wanawasiliana bila kuwepo na viziada lugha. Katika mitandao hii, washiriki wana uwezo wa kuzua kaida za maingiliano na hata njia za kusuluhisha shida yoyote kati yao.

Herring (2001) anadokeza kuwa mawasiliano ya kimtandao yanaweza kutumiwa kama eneo la kupata data za utafiti ikiwa mtandao husika ni wazi na unaweza kuufikiwa na kila mtu pasi na nambari za siri au nywila kuhitajika kuufikia. Herring (khtj) hivyo anafananisha mtandao wa aina hii na hali ya kukusanya data kutoka kwa mkahawa kwa kutazama. Sifa kuu inayojitokeza katika mawasiliano ya kimtandao ni uhuru uliopo wa kujieleza bila kudhibitiwa. Sproull na Kiesler (khtj) wanaeleza uhuru wa kutodhibitiwa katika mawasiliano ya kimtandao kama hali ya kuchukua kiapo. Kim na Raja (1991) wanauchukulia uhuru huu wa kutodhibitiwa kama kutukanana, kutoa kauli hasiri au kutoa lawama.

Kulingana na Smolensky na wengine (1990) watu ambao hawajuani wana kiwango kikubwa cha kujieleza bila kudhibitiwa. Naye Boshier (1990) anasema kuwa uhuru wa kutodhibitiwa katika maelezo unatokea kutokana na masafa ya kimaeneo kati ya mzungumzaji na msikilizaji iwapo si mazungumzo ya ana kwa ana. Hata hivyo, anaeleza kuwa tabia hii hubadilika iwapo mzungumzaji na msikilizaji wataendeleza mawasiliano ya ana kwa ana.

**3.2 Diskosi ya Siasa katika Nchi ya Kenya**
Barasa (2014) akimnukuu King'ei (2000) anaeleza kuwa diskosi ya siasa katika nchi ya Kenya inahusisha lugha ya kuelekeza, kudhibiti na kuwachochea wafuasi katika njia fulani ya kisiasa. Diskosi ya siasa katika nchi ya Kenya inahusishwa na sifa mbalimbali. Kwanza, kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi kumechangia kutokea kwa ushindani mkali wa kisiasa ambapo vyama vya kisiasa hutumia njia mbalimbali ili kuibuka na ushindi. Ushindani huu umechangia kuzuka

kwa siasa za kikabila ambapo ufuasi wa kisiasa unategemea kabila la mhusika.
Kuondolewa kwa sehemu ya 2A ya katiba katika mwaka wa 1992 katika nchi ya Kenya kulichangia kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi ambavyo vilishindana katika chaguzi. Mfumo huu wa vyama vingi umechangia kuzuka kwa ushindani mkali wa kisiasa jambo ambalo limesababisha kutokea kwa siasa hasi

Sifa kuu inayohusishwa na diskosi ya siasa katika nchi hii ni kuingizwa kwa ukabila katika siasa. Barasa (2014) akimnukuu Kimenyi (2008), alidhihirisha kuwa kuingizwa kwa ukabila katika siasa kumechangia kutokea kwa ghasia za kikabila zinazoshuhudiwa nchini. Kimenyi (khtj) anaeleza kuwa ghasia za kisiasa nchini zinachochewa na lugha inayotumiwa na wadau katika diskosi hii ambapo lugha hii hutumiwa kuchochea kabila fulani dhidi ya jingine. Uchochezi huu hutekelezwa kwa semi za chuki.

Utafiti unaonyesha kuwa juhudi za kutumia teknolojia katika kuendeleza shughuli za serikali nchini Kenya zilianzishwa na rais mstaafu Mwai Kibaki katika mwaka wa 2006. Katika hotuba yake, rais Kibaki alieleza kuwa maendeleo ya nchi yoyote hutegemea upatikanaji wa habari. Hali hii ilichochea kuzinduliwa kwa mfumo wa kidijitali katika shughuli za serikali. Siasa ni mojawapo ya mawanda ya serikali iliyofaidika na mfumo huu. Hata hivyo, kuingizwa kwa teknolojia katika siasa kumekuja na madhara mbalimbali.

Madhara ya teknolojia katika siasa yalidhihirika katika uchaguzi wa mwaka wa 2007 ambapo vyombo vya habari vilihusika katika kueneza semi za chuki miongoni mwa wananchi. Kutokea kwa ghasia za baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2007/08 kulifanya serikali kubuni mikakati mbalimbali ili kudhibiti semi za chuki zilizoendelezwa kwenye vyombo vya habari na kwenye majukwaa ya kisiasa. Kulingana na ripoti ya Waki (2008), wanasiasa, wataalamu wa kisiasa pamoja na vyombo vya habari vilichangia kutokea kwa hali ya atiati nchini Kenya kwa kuendeleza jumbe za chuki.

Hali hii ilifanya serikali kudhibiti vyombo vya habari ili kuhakikisha kuwa semi na jumbe za chuki hazikutolewa na vyombo hivi. Kutokana na hali hii, semi za chuki ziliingizwa kwenye mitandao ya kijamii kama vile *Facebook* na *Twitter*. Kwa mfano, katika uchaguzi wa mwaka wa 2017, kauli nyingi za uchochezi na za vitisho ziliripotiwa kutumika katika mitandao ya kijamii. Uhasama wa kikabila nchini unadhihirika zaidi kupitia mitandao ya kijamii. Wafuasi wa vyama mbalimbali wanazidi kushambuliana kwa kutumia semi za uchochezi na za chuki kupitia mitandao ya kijamii.

### 3.3 *Facebook* na Diskosi ya Siasa

*Facebook* ni mojawapo ya mitandao ya kijamii ambayo inatumiwa na watu wengi duniani kote. Mtandao huu uliasisiwa na Mark Zukerberg katika mwaka wa 2014. Mtandao huu ulianza kama ukumbi uliotumiwa na wanafunzi wa vyuo vikuu kule Mrekani wa kubadilishana picha na jumbe mbalimbali. Kulingana na Westling (2007) kwa kuwa ukumbi huu ulikuwa wazi na ulihitaji tu anwani ya barua pepe kujisajili, uanachama wake uliongezeka duniani kote. Mtandao huu unashabikiwa na vijana sana kwani wengi wao wanautumia kama chanzo cha burudani.
Kulingana na Dwyer na wenzake (2007) mtandao wa *Facebook* unatumiwa na watu kutekeleza shughuli mbalimbali kama vile kuendeleza biashara, kukutana na marafiki, kutafuta wachumba na kadhalika.

Katika diskosi ya siasa, mtandao wa *Facebook* umeweza kutumiwa na wanasiasa

kuendeleza kampeni zao mbali na kutumiwa na wananchi kupiga kura hususan katika mataifa yenye demokrasia kamavu kama vile Marekani. Wanasiasa hutumia mtandao huu kunadi sera zao kwa kuwaeleza wapiga kura yale waliyoyafanya na ambayo wangependa kutekeleza mbeleni. Wengi wa wanasiasa hutumia mtandao huu kuwafikia wapiga kura vijana ambao ndio watumizi wakuu wa *Facebook*. Leo hii, wanasiasa huandika jumbe zenye masuala kadhaa katika kurasa zao za Facebook ili wafuasi wao wazisome na kuzitolea maoni. Wafuasi wao hutoa maoni yao kuhusu masuala hayo kwa kutoa kauli zao.

Baadhi ya vipengele vya *Facebook* vinavyofanikisha hali hii ni kama vile 'makundi' na 'shughuli'. Makundi haya yanaweza kuwa wazi au funge. Makundi wazi ni yale ambayo kila mshiriki anaweza kujiunga nayo na hivyo hakuna nywila yoyote inayohitajika ili mtu ajiunge nayo. Hata hivyo, makundi funge ni yale ambayo wanaoruhusiwa kujiunga nayo ni wale waalikwa pekee. Hivyo, si kila mshiriki anaweza kujiunga na makundi funge. Kila kundi lina msimamizi ambaye aghalabu ndiye aliliyanza. Msimamizi huyu hudhibiti na kuongoza yanayotendeka katika makundi hayo.

Washiriki katika makundi haya wana nafasi ya kutoa maoni yao kuhusu masuala yanayojadiliwa kwayo. Wengi wa wanasiasa wana makundi katika *Facebook* ambayo wanatumia kutagusana na wafuasi wao. Kupitia makundi hayo, washiriki wanaweza kupitisha jumbe zao moja kwa moja kwa wanasiasa hao. Jumbe hizi zitaweza kusomwa na kila mshiriki katika kundi husika.

Jumbe nyingi zinazotumwa katika makundi haya zinawapongeza wanasiasa au huwa za kutaka habari fulani kutoka kwao. Hata hivyo, baadhi ya jumbe hizo zinabeba hisia zenye utopole ambazo zinalenga kuhasiri uso wa mwanasiasa husika au washiriki wengine. Jumbe hizi hasi zinaweza kumfanya mwanasiasa huyu kutaka kufunga ukurasa huo ingawa kufunga huko kutamfanya awapoteze wafuasi wake jambo ambalo hakuna mwanasiasa analitaka. Westling (2007) ansema kuwa mtandao wa *Facebook* unaendeleza na kudumisha diskosi ya siasa na kuwa una uwezo wa kuwa njia muhimu ya diskosi ya siasa.

Kulingana na Ndavula (2013), nchini Kenya, mitandao ya kijamii inatumiwa sana katika diskosi ya siasa ambapo kati ya mitandao yote ya kijamii, mtandao wa *Facebook* unatumiwa na wanasiasa sana. Katika uchaguzi wa mwaka wa 2017, zaidi ya asilimia 80 ya wagombezi wa viti mbalimbali vya kisiasa walitumia mitandao ya kijami kuendeleza kampeni zao. Takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 90 ya wakenya wanatumia mitandao mbalimbali ya kijamii huku asilimia 80 ya wakenya hao wakitumia mtandao wa *Facebook*.

Katika utafiti wao, Goldstein na Rotich (2008) walionyesha kuwa mitandao ya kijamii nchini Kenya inatumiwa sana katika kueneza uvumi, ghasia, semi za chuki na kuendeleza chuki za kisiasa miongoni mwa wakenya. Wanaeleza kuwa wanasiasa hutumia mitandao hii kuwahamasisha wafuasi wao na kuwaeleza wafuasi wao matukio kadhaa ya kisiasa yanayoendelea nchini. Miongoni mwa wanasiasa wanaotumia mtandao wa *Facebook* ni Raila Odinga na William Ruto. Kurasa zao za *Facebook* zinaonyesha kuwa kila mmoja anafuatwa na wakenya zaidi ya milioni 1.4.

Utafiti huu ulichagua mtandao wa *Facebook* kuchunguza diskosi ya siasa kwa sababu ya uasilia wake katika uwasilishaji wa jumbe. Data zilizochanganuliwa kutoka kwa mtandao huu basi ni zile zilizotokana na diskosi katika muktadha halisi wa mazungumzo. *Facebook* pia ilichaguliwa na mtafiti kutokana na urahisi wake kimatumizi mbali na kutokuwepo na vikwazo

katika kujiunga na ukurasa husika. Kando na hayo, mtafiti aliuchagua mtandao wa *Facebook* kwa sababu ndio mtandao wa kijamii unaotumiwa na wanasiasa wengi katika kuendeleza siasa zao.

**3.4 Yaliyoandikwa kuhusu Ukiukaji wa Kanuni za Ushirikiano za Grice (1975)**

Davies (2007) anaeleza ushirikiano kama dhana inayotumiwa katika isimu kuonyesha tabia ya binadamu katika mazungumzo. Leech (2011) anasema kuwa mzungumzaji anahitaji kanuni za ushirikiano ili kufasiri uhusiano kati ya maana na mamlaka. Tafiti kadhaa kuhusu kanuni za ushirikiano zimetekelezwa na watafiti mbalimbali kama vile Arthanti (2013) ambaye alitafiti utafiti wenye mada '*Violations of Grice's maxims in the Gartified 'Hangs Out' Comic: Comparison between Source Text (ST) and Target Text (TT)'*.

Katika utafiti huu, mtafiti huyu alichunguza ukiukaji wa kanuni za ushirikiano katika matini changizi na kama ukiukaji huo pia hufanyika katika matini lengwa. Utafiti huu ulikuwa elezi. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kuwa si kanuni zote hukiukwa katika matini lengwa. Utafiti huu ni tofauti na utafiti wetu kwa kuwa ulichunguza ukiukaji wa kanuni za ushirikiano katika fasihi ilhali utafiti wetu ulichunguza ukiukaji wa kanuni za ushirikiano katika diskosi ya siasa katika mtandao wa *Facebook*. Hata hivyo, utafiti huu ni muhimu katika kufanikisha uchanganuzi wa data za ukiukaji wa kanuni za ushirikiano katika utafiti huu.

Junaredi (2017) aliendeleza utafiti wenye mada '*The Violation of Cooperative Principles through Gender Language features in 'Love, Rosie film'*. Mtafiti huyu alitaka kuchunguza uhusiano uliopo kati ya kanuni za ushirikiano na sifa za lugha jinsia katika filamu hiyo. Utafiti huu ulikuwa elezi na mtafiti alikusanya data zake kwa kurekodi kauli za wahusika. Matokeo yake yalionyesha kuwa wahusika hukiuka sana kanuni ya namna katika filamu hiyo. Utafiti huu pia ulijikita katika fasihi ilhali utafiti wetu ulijikita katika diskosi ya siasa inayofanyika katika mtandao wa *Facebook*. Utafiti huu ni muhimu kwa utafiti wetu katika kuuwekea msingi wake kinadharia.

Anneke (2008) katika utafiti wake wenye mada *'The Multiple Violations of Conversational Maxims in Lying done by the characters in some episodes of Desperate Housewives'* alichunguza idadi ya wahusika katika filamu hiyo waliokiuka kanuni za ushirikiano wanapodanganya. Utafiti wake ulionyesha kuwa kanuni zote za ushirikiano zilikiukwa na wahusika ili kuhitimisha mazungumzo, kuficha ukweli au kudanganya. Utafiti huu ulishughulikia ukiukaji wa kanuni za ushirikiano wahusika wanapodanganya katika fasihi tofauti na utafiti wetu ambao ulishughulikia ukiukaji wa kanuni za ushirikiano katika diskosi ya siasa miongoni mwa washiriki wa mtandao wa *Facebook* nchini Kenya. Utafiti huu ulitusaidia katika kuupa utafiti wetu msingi wake kinadharia.

Katika makala yake '*The Violation of Cooperative Principle and four Maxims in Iranian Psychological Consultation*', Arezou (2014) alichunguza jinsi kanuni za ushirikiano zinakiukwa katika ushauri wa kisaikolojia unaotolewa nchini Iran. Mtafiti huyu alibaini kuwa ukiukaji huu hutokana na ugumu wa shughuli yenyewe. Utafiti huu ni tofauti na utafiti wetu kwa kuwa ulishugulikia mawasiliano ya ana kwa ana ilhali utafiti wetu ulichunguza jinsi kanuni za ushirikiano zinakiukwa katika diskosi ya siasa miongoni mwa washiriki wa mtandao wa *Facebook* nchini Kenya. Hata hivyo, utafiti huu ni muhimu katika kuupa utafiti wetu msingi wake kinadharia.

Putra (2014) alifanya utafiti wenye mada '*The Grice's Cooperative Principle in the transcript of Beyonce interview on 'Pilers Morgan Tonight'*. Katika utafiti huu, mtafiti huyu alibainisha kuwa

wahusika wote wawili walikosa kuzingatia kanuni za ushirikiano katika kauli zao. Utafiti huu ulishughulikia ukiukaji wa kanuni za ushirikiano katika mawasiliano ya ana kwa ana tofauti na utafiti wetu ambao ulishughulikia ukiukaji wa kanuni za ushirikiano katika mtandao wa *Facebook*. Hata hivyo, utafiti huu ni muhimu katika kuendeleza nadharia ya utafiti.

Dewanata (2018) katika utafiti wake '*The Analysis of Grice's Cooperative Principles on the Responses of Indonesian Politicians: Prag matic study*', alichunguza jinsi kanuni za ushirikiano zinakiukwa katika mahojiano ya kisiasa na jinsi ukiukaji huo unachangia katika kujenga ajenda za mwanasiasa. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa wanasiasa hao hukiuka kanuni za ushirikiano ili kukinga nyuso zao mbali na kuendeleza ajenda zao. Utafiti huu ni tofauti kwa kuwa ulijikita katika diskosi ya siasa katika mawasiliano ya ana kwa ana ilhali utafiti wetu ulishughulika na ukiukaji wa kanuni za ushirikiano katika diskosi ya siasa katika mtandao wa *Facebook*. Hata hivyo, utafiti huu ni muhimu katika uchanganuzi wa data.

Mapitio haya ya mandishi kuhusu ukiukaji wa kanuni za ushirikiano yanadhihirisha wazi kuwa tafiti kuhusu ukiukaji wa kanuni za ushirikiano zimeendelezwa sana katika nchi za magharibu kuliko za Afrika. Mapitio hayo pia yanaonyesha kuwa utafiti kuhusu ukiukaji wa kanuni za ushirikiano katika diskosi ya siasa inayofanyika katika mtandao wa *Facebook* haujashughulikiwa. Hili ni pengo ambalo utafiti huu ulilenga kuziba.

**4.0 Misingi ya Kinadharia**

Utafiti huu uliongozwa na

Kanuni za Ushirikiano za Grice (1975). Kanuni za ushirikiano zinatokana na nadharia ya Umaanisho iliyoasisiwa na Grice (1975). Kulingana na Levinson (1983) nadharia ya Umaanisho inahusika na jinsi maana inawasilishwa kupitia kwa yanayowasilishwa pamoja na jinsi inasemwa.

Kulingana na nadharia hii, kuna kanuni za ushirikiano zinazoongoza mazungumzo na ambazo zinaongoza namna lugha inafaa kutumiwa. Kanuni hizi zinaaminika kuwa na umuhimu kimantiki na kisemantiki kwa kuwa zinadhihirisha kanuni ya umaanisho (Levinson, 1983). Yule (1996) huchukulia kanuni za ushirikiano kama fikra zisizowasilishwa katika muktadha wa mazungumzo. Grice (1975) anazichukulia kama kanuni bia ingawa Abdul-Wahid (2000) huzichukulia kama zinazoongozwa na mila hususan kanuni za kiasi na ukweli. Grice (1975) anadai kuwa ushirikiano katika mazungumzo humaanisha kuwa kila mzungumzaji anaelewa kuwa kila tamko huweza kuwa na athari kwa nyuso za wengine. Hii ndiyo maana lazima wazungumzaji wadhibiti matamko yao kwa njia fulani ili mazungumzo yao yawe na upole.

**4.1 Mihimili ya nadharia ya Kanuni za Ushirikiano**

Kulingana na Grice (1975), kanuni za ushirikiano ni desturi ambazo huongoza mawasiliano na zisipofuatwa na wazungumzaji hali ya utopole hudhihirika katika mchakato wa mawasiliano. Hizi kanuni ni kama vile:

**Kanuni ya Kiasi**

Kanuni hii humhitaji mzungumzaji kutoa habari inayohitajika tu. Kulingana na kanuni hii, mzungumzaji hafai kutoa habari zaidi ya inayohitajika, kwa hivyo, mzungumzaji akitoa habari chache au nyingi zaidi ya inayohitajika anaweza kukiuka uso wa msikilizaji jambo

linalosababisha kuwepo kwa utopole. Hali hii hudhihirika zaidi katika diskosi ya kisiasa.

**Kanuni ya Ukweli**

Kanuni hii humhitaji mzungumzaji kujaribu kutoa kauli zenye ukweli. Mzungumzaji anahitajika kutoa kauli ambazo zinaweza kuthibitika na ambazo ana ushahidi wa kutosha.

**Kanuni ya Uhusiano**

Katika kanuni hii, mzungumzaji anahitajika kuzingatia muktadha wa mazungumzo anapotoa habari yoyote. Mzungumzaji anahitajika kutozungumzia habari zilizo nje ya mada ya mazungumzo.

**Kanuni ya Namna**

Katika kanuni hii, mzungumzaji anahitajika kuepukana na utata anapozungumzia habari fulani na awe na mpangilio katika mazungumzo yake. Mzungumzaji anafaa kutoa habari zake kwa namna inayoeleweka vizuri na kwa njia wazi. Hali hii humsaidia msikilizaji kuweza kuitikia habari iliyotolewa kwa njia iliyokusudiwa na mzungumzaji.

**4.2 Ukiukaji wa Kanuni za Ushirikiano za Grice (1975)**

Ingawa kanuni hizi huchangia kuwepo kwa ushirikiano katika mazungumzo, aghalabu kanuni hizi hazifuatwi na wazungumzaji kama alivyopendekeza Grice (1975). Kulingana na Grice (1975), ukiukaji wa kanuni za ushirikiano hutokea iwapo wazungumzaji watakosa kimaksudi kuzitumia katika mazungumzo yao ili kusababisha kutoelewana kati yao au kutimiza malengo mengine.
Kulingana na Grice (1975), ufuataji na uzingativu wa kanuni za ushirikiano unatekelezwa na mzungumzaji kwa hiari yake kwani unalenga kumfaidi mwenyewe mbali na kuonyesha umilisi wake wa lugha. Kulingana naye, ingawa kanuni hizi zinafaa kufuatwa na wazungumzaji katika mazungumzo, kuna miktadha ambamo kanuni hizi hazifuatwi wala kuzingatiwa na wazungumzaji na hivyo zinakiukwa. Hata hivyo, Grice (1975) anaeleza kuwa licha ya ukiukaji huu, mawasiliano hayataathiriwa kwani kanuni hizo huchangia tu kuwepo kwa muwala na mfululizo wa mazungumzo.

Leech (1980) anaeleza kuwa wazungumzaji hujaribu kufasiri maana iliyowasilishwa katika mazungumzo licha ya kanuni hizo kukiukwa. Anaeleza kuwa wazungumzaji hujaribu kuteua maana faafu kutoka kwa kauli iliyotolewa mbali na kutumia umaanisho kupata maana lengwa. Palupi (2006) anaeleza kuwa kanuni za ushirikiano za Grice (1975) si kanuni za kisayansi ambazo haziwezi kukiukwa ila ni miongozo inyoongoza mazungumzo. Levinson (1983) anaeleza kuwa Grice (1975) anaelewa kuwa wazungumzaji wanaweza kupuuza kanuni za ushirikiano ingawa kupuuza huku hakuwezi kukiuka upitishaji wa ujumbe kwani kanuni za ushirikiano huleta muwala katika mazungumzo.

**Jedwali 1: vipengele vya ukiukaji wa Kanuni za Ushirikiano kulingana na Grice (1975)**

| Kanuni za ushirikiano | Vipengele vya ukiukaji |
|---|---|
| **Kanuni ya kiasi** | • Mzungumzaji kutoa habari chache kuliko zinazohitajika<br>• Mzungumzaji kutoa habari nyingi zaidi ya inayohitajika<br>• Mzungumzaji kurudia habari nyingine |
| **Kanuni ya ukweli** | • Mzungumzaji kutosema ukweli<br>• Mzungumzaji kutoa kauli yenye kinaya au kejeli<br>• Mzungumzaji kukataa kauli fulani<br>• Mzungumzaji kuvunja habari husika |
| **Kanuni ya uhusiano** | • Mzungumzaji kuzungumzia hoja isiyohusiana na mada ya mazungumzo.<br>• Mzungumzaji kugeuza mada ya mazungumzo ghafla.<br>• Mzungumzaji kukosa kuzungumzia hoja fulani<br>• Mzungumzaji kusababisha matokeo hasi kutokea |
| **Kanuni ya namna** | • Mzungumzaji kutumia kauli tata<br>• Mzungumzaji kutia chumvi kauli zake<br>• Mzungumzaji kutumia misimbo kwa wasioifahamu |

## 5.0 Muundo na Mbinu za utafiti

### 5.1 Eneo la utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika muktadha wa Kenya ambapo mtafiti alichunguza ukiukaji wa kanuni za ushirikiano katika diskosi ya siasa kuanzia Januari 1 hadi Aprili 30, 2021. Uchunguzi huu ulihususha utafiti wa mtandaoni na maktabani. Utafiti wa mtandaoni ulitumiwa na mtafiti kukusanya kauli za washiriki kutoka kwa kurasa za *Facebook* za wanasiasa Raila Odinga na William Ruto. Utafiti wa maktabani ulimhitaji mtafiti kusoma tafiti kadhaa zenye masuala ya kanuni za ushirikiano, kusoma vitabu pamoja na makala mbalimbali kama vile gazeti la *Taifa Leo*.

### 5.2 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ni wa kistahilifu na unahusisha utafiti wa mtandaoni na maktabani. Kulingana na Mugenda na Mugenda (2005) utafiti wa kistahilifu unahusu uchanganuzi wa vitu katika hali zao asilia na kujaribu kufasiri maana ambayo wanajamii huvipa vitu hivyo. Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo. Data za utafiti huu ni kauli za washiriki katika kurasa za *Facebook* za wanasiasa Raila Odinga na William Ruto. Utafiti huu ulichagua kurasa hizi kama vyanzo vya data ili kuzua uhalali wa data mbali na kuondoa upendeleo wa mtafiti ambao ungetokea kama mtafiti angetumia ukurasa mmoja wa *Facebook* kama chanzo cha data. Utafiti huu ulitumia mbinu ya uchanganuzi matini katika kuchanganua kauli ya siasa. Kipashio cha uchanganuzi ni kauli ya siasa.

### 5.3 Usampulishaji na Sampuli

Katika utafiti huu, tulitumia sampuli kusudio ili kuteua kauli ya siasa iliyojumuisha data ya utafiti. Kauli hii iliteuliwa kwa kuzingatia uwezo wake wa kujibu swali la utafiti. Kauli zilizoshirikishwa katika utafiti huu ni zile zilizowekwa katika kurasa hizo za *Facebook* kati ya

Januari 1 hadi Aprili 30, 2021. Kipindi hiki kilishuhudia matukio mengi ya kisiasa yakiwemo juhudi za kubadilisha katiba kupitia mswada wa BBI mbali na kuzuka kwa mirengo tofauti ya kisiasa. Kulingana na Gall na wenzake (1996) lengo la kutumia sampuli kusudio ni kuteua watafitiwa au vitu vya kutafiti ambavyo vina habari za kutosha katika muktadha wa utafiti elezi. Naye Creswell (2013) anaeleza kuwa sampuli kusudio hutumiwa katika utafiti elezi ili kumwezesha mtafiti kuteua washiriki na mahali pa kufanyia utafiti kwa sababu ya uwezo wao wa kueleza suala linalotafitiwa.

Nduva (2016) anaeleza kuwa lengo la idadi ya sampuli katika utafiti elezi ni kutoa ufafanuzi wa kutosha kuhusu suala linalochunguzwa. Holloway na Wheeler (2002) nao wanaeleza kuwa katika utafiti elezi, idadi ya sampuli haiathiri umuhimu na thamani ya utafiti husika. Hii inamaanisha kuwa ubora wa matokeo ya utafiti hautegemei sana idadi ya sampuli iliyochanganuliwa lakini hutegemea kiwango cha uchanganuzi.

Holloway na Wheeler (2002) wanaongeza kuwa hakuna mwongozo maalum unaofuatwa katika kubaini idadi ya sampuli katika utafiti wa kistahilifu. Hii ni kwa sababu watafiti katika tafiti za kistahilifu hawana uhakika wa idadi ya kundi lengwa kabla utafiti kufanywa mbali na sampuli kubadilika katikati ya utafiti. Kulingana na Polkinghorne (2005), katika utafiti wa kistahilifu, haja kuu sio idadi ya sampuli itakayokusanywa au kutoka kwa vyanzo vingapi bali ni uwezo wa data itakayokusanywa kutimiza malengo ya utafiti. Sampuli katika utafiti huu ni kauli 85 ambazo zilichanganuliwa ili kutimiza lengo la utafiti.

**5.4 Vifaa vya Kukusanyia Data**

Mtafiti alitumia wi-fi, simu, tarakilishi, kalamu na karatasi katika kukusanya data. Mtafiti alitumia simu na tarakilishi kuingia kwenye kurasa za *Facebook* za wanasiasa hao. Wi-fi ilimsaidia mtafiti kusakura mtandao wa *Facebook*. Mtafiti alitumia kalamu na karatasi kunakili kauli za washiriki.

**5.5 Mbinu za Kukusanya Data**

Katika kukusanya data mtafiti alitumia mbinu za kunakili, kusoma magazeti hasa gazeti la *Taifa Leo* na tasnifu mbalimbali ili kuyadurusu yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti. Mbinu ya kunakili ilitumiwa na mtafiti kurekodi data za utafiti kutoka kwa kurasa za *Facebook* za wahe. Raila Odinga na William Ruto. Pia, mtafiti aliyadurusu machapisho kama vile magazeti yaliyo na masuala yaliyotafitiwa katika utafiti huu ili kuhalalisha data zilizokusanywa kutoka kwa kurasa husika. Data ya utafiti ilikusanywa kutoka kwa kurasa mbili za *Facebook*: ukurasa wa *Facebook* wa mhe. Odinga na wa mhe. William Ruto. Mbinu hizi zilimwezesha mtafiti kupata data nyingi za utafiti bila kukabiliana na changamoto za kutazama kutoka kwa washiriki (Bousfield, 2008).

**5.6 Utaratibu wa Kukusanya Data**

Baada ya kupata kibali cha utafiti, mtafiti alijaribisha vifaa vyake vya kukusanya data ili kuhakikisha kuwa vinamfaa. Kwa kuwa *Facebook* ni mtandao wazi, ili kujiunga na ukurasa wa *Facebook* wa mhe. Odinga, mtafiti alitafuta jina 'Raila Odinga' katika ukurasa wake wa *Facebook* jambo ambalo lilimwezesha kuwa mmoja wa wanaomfuata katika mtandao huo. Hatua hii ilirudiwa ili kumwezesha mtafiti kujiunga na ukurasa wa *Facebook* wa mhe. William Ruto.

Raila Odinga ni mwanasiasa wa upinzani nchini Kenya ambaye kulingana na Badejo (2006) ni mwanasiasa anayedhibiti siasa katika nchi ya Kenya. Naye William Ruto, hadi wakati wa kuandika makala hii, ni naibu wa rais katika nchi ya Kenya. Mtafiti alichagua kurasa zao za *Facebook* kwa sababu kadhaa: kwanza, kurasa zao za *Facebook* ni kati ya kurasa ambazo zinawafuasi wengi mtandaoni, hivyo, mtafiti angepata data nyingi kutoka kwazo.

Pia, hulka za mhe. Odinga zilimsukuma mtafiti kuchagua ukurasa wake wa *Facebook*. Sifa zake za wakati mmoja kuunga mikono serikali na wakati mwingine kuipinga serikali zilimfanya mtafiti kuamini kuwa kungekuwa na sasisho zake ambazo wakati mmoja ziliunga mikono serikali na wakati mwingine kuipinga. Hali hii iliufanya ukurasa wake wa *Facebook* kuwa muhimu zaidi kuliko kurasa nyingine.

Ukurasa wa *Facebook* wa mhe. William Ruto ulikuwa muhimu hususan kwa kipindi cha utafiti kwani kipindi hicho kilishuhudia mabadiliko ya kisiasa hususan baada ya handsheki iliyofanyika kati ya rais Uhuru Kenyatta na mhe. Odinga. Mabadiliko haya yalionekana kutomridhisha mhe. Ruto jambo lililomfanya kuanza kupinga shughuli nyingi za serikali licha ya kuwa naibu wa rais. Kutokana na hali hii, inaaminika kuwa angeweza kudhihirisha misimamo yake ya kisiasa kwa wafuasi wake hususan kupitia mitandao yake ya kijamii, *Facebook* ukiwemo. Baada ya kuingia katika mitandao hiyo mtafiti aliteua sasisho tano zilizowekwa kati ya Januari 1 hadi Aprili 30, 2021 ambazo kupitia kwazo, data za utafiti zilikusanywa. Sasisho hizi ziliteuliwa kimakusudi. Mtafiti alianza kukusanya data kwa kupitia kauli zilizowekwa na washiriki akiwa na lengo la kuzisoma na kuzielewa.

Mtafiti baadaye alinakili data za utafiti zilizodhihirika katika kauli zilizopitiwa. Baada ya kunakili data za utafiti, mtafiti alizipa misimbo ya kuzitambulisha. Hatua ya mwisho ilimhitaji mtafiti kuainisha data zilizokusanywa katika kategoria mbalimbali kutegemea mihimili ya nadharia ya utafiti.

**5.7 Uchanganuzi wa Data**

Mtafiti alitumia uchanganuzi matini kuchanganua data kwa sababu alilenga kutoa maelezo kuhusu suala lililotafitiwa. Mbinu ya uchanganuzi matini ilitumiwa na mtafiti kwa sababu utafiti huu ulilenga kuchunguza sifa ya lugha inayotumiwa katika mawasiliano ya kimtandao ili kuipa maana katika muktadha husika. Uchanganuzi matini una uwezo wa kuchanganua na kuzua maana kutoka kwa data na baadaye kutoa mahitimisho kutokana na data zilizokusanywa. Uchanganuzi wa data ulifanywa kulingana na lengo la utafiti na mihimili ya nadharia ya utafiti. Enon (1998) anasema kwamba huu ni uchanganuzi unaomhitaji mtafiti kuzitolea data zake maelezo.

Data ya utafiti ilichanganuliwa kwa kufuata hatua tatu: kwanza, uainishaji wa kauli kwa kuzingatia uamilifi wao katika kategoria mbalimbali za lengo la utafiti; pili, ufasiri wa uamilifu wa kila kauli iliyonakiliwa na mwisho kutoa maelezo kuhusu uamilifu wa kauli zilizokusanywa kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya utafiti. Uchanganuzi huu ulihusisha kanuni za ushirikiano zilizokiukwa na washiriki wa mtandao wa *Facebook* katika diskosi ya siasa nchini Kenya. Vipengele vya ukiukaji wa kanuni za ushirikiano viliongoza uchanganuzi huu.

**6.0 Matokeo ya Utafiti: Uchanganuzi wa Kanuni za Ushirikiano zinazokiukwa na washiriki wa mtandao wa *Facebook* katika diskosi ya siasa nchini Kenya.**

Kulingana na Grice (1975), ukiukaji wa kanuni za ushirikiano hutokea iwapo wazungumzaji watakosa kimaksudi kuzitumia katika mazungumzo yao ili kusababisha kutoelewana kati yao au kutimiza malengo mengine. Kulingana na Grice (1975) mzungumzaji anaweza kukosa kuonyesha ushirikiano kwa sababu ya mgongano wa kanuni za ushirikiano. Mgongano wa kanuni huweza kutokea wakati msemaji anaona ugumu kufuata kanuni mbili au zaidi kwa pamoja.

Katika utafiti huu, mtafiti aliweza kukusanya kauli 85 ambazo zilidhihirisha ukiukaji wa kanuni za ushirikiano. Kauli hizi zilichanganuliwa kwa kutumia nadharia ya Kanuni za Ushirikiano ya Grice (1975) kupitia kwa mhimili wake wa kanuni za ushirikiano. Mtafiti alitumia vipengele vya ukiukaji wa kanuni za ushirikiano zilizopendekezwa na Grice (1975).

Jedwali: Umaratokezi wa Kanuni za Ushirikiano zilizokiukwa

| Kanuni ya ushirikiano | Umaratokezi wa ukiukaji | Asilimia |
|---|---|---|
| **Kanuni ya kiasi** | 28 | 32.9 |
| **Kanuni ya uhusiano** | 21 | 24.7 |
| **Kanuni ya Ukweli** | 22 | 25.9 |
| **Kanuni ya namna** | 14 | 16.5 |
| **Jumla** | 85 | 100 |

Jedwali hili linaonyesha kuwa washiriki wa mtandao wa *Facebook* hukiuka zaidi kanuni ya kiasi kwa asilimia 32.9. Mtafiti aliweza kubainisha kauli 28 za washiriki wa mtandao wa *Facebook* zilizokiuka kanuni ya kiasi. Matokeo haya ni sawa na matokeo ya utafiti uliofanywa na Ayunon (2018) yaliyoonyesha kuwa washiriki katika mtandao wa *Facebook* hukiuka kanuni ya kiasi kwa asilimia kubwa kuliko kanuni nyingine. Aghalabu washiriki wa mtandao wa *Facebook* husasisha hali zao kwa kutoa kauli ambazo hazieleweki kikamilifu kwa sababu ya habari chache au nyingi zaidi zinazojitokeza katika kauli hizo. Kanuni hii ilifuatwa na kanuni ya ukweli ambayo ilikiukwa na washiriki wa mtandao wa *Facebook* kwa asilimia 25.9. Kanuni za uhusiano na namna zilijitokeza kwa asilimia 24.7 na 16.5 mtawalia.

Utafiti ulibainisha kuwa kwa kuwa mijadala iliyopo ilikuwa ya siasa, washiriki walijikita katika kutoa maelezo mengi sana ambayo hayakuwa muhimu kwa diskosi husika. Kulingana na Ayunon (2018), kwa kawaida, wazungumzaji hukiuka kanuni za ushirikiano ili watimize malengo fulani kama vile kuingiza ucheshi au kejeli kwenye kauli zao. Hata hivyo, si kanuni zote za ushirikiano zilikiukwa na washiriki wa mtandao wa *Facebook* katika sasisho zote. Baadhi ya sasisho hazikudhihirisha ukiukaji wa baadhi ya kanuni za ushirikiano.

**6.1 Ukiukaji wa Kanuni ya Kiasi**

Kanuni ya kiasi humhitaji mzungumzaji kutoa habari zinazohitajika tu. Kulingana na kanuni hii, mzungumzaji hafai kutoa habari chache au nyingi zaidi ya zinazohitajika katika mchakato wa mawasiliano. Kulingana na Grice (1975) kanuni ya kiasi hukiukwa ikiwa mzungumzaji atatoa habari nyingi zaidi ya zinazohitajika au habari chache kuliko zinazohitajika. Pia, kanuni hii hukiukwa ikiwa mzungumzaji atarudia habari fulani katika mchakato wa mawasiliano. Kupitia

vipengele hivi, mtafiti aliweza kukusanya kauli za washiriki 28 ambazo zilikiuka kanuni hii. Utafiti ulibainisha kuwa washiriki wa mtandao wa *Facebook* wanaposasisha kauli zao, wanatoa habari nyingi zisizo na maudhui bayana. Hali hii ilidhihirika zaidi kwa sababu utafiti huu ulihusisha diskosi ya siasa ambayo inahusisha matumizi ya maneno ili kuwarai raia wakuunge mikono au kuwasuta wapinzani. Hata hivyo, utafiti pia ulibainisha kuwa wakati mwingine, washiriki wa mtandao wa *Facebook* hutoa habari chache ambazo huwaacha wasikilizaji wao na maswali mengi kuhusu mada ya mazungumzo. Kanuni hii ilikiukwa kwa njia zifuatazo:

Sasisho ya 1 (Januari 27, 2021)

(*Sasisho hii ilitolewa kutoka kwa ukurasa wa Facebook wa mhe. Odinga baada ya kuzuru eneo la Githurai ambalo liko katika eneo la kati nchini Kenya. Eneo hili linaaminika kuwa halijawahi kuunga mkono azma ya mhe. Odinga ya kuwania urais. Pia, kabla ya ziara hii, kulikuwa na hali ya wasiwasi ya kisiasa iliyoripotiwa katika eneo hili, hususan kupitia semi za kisiasa zilizoripotiwa katika mitandao ya kijamii ambapo baadhi ya semi hizo zilikuwa zikimuonya dhidi ya kuzuru eneo hilo.*)

> Leo nimefurahi kuzuru na kujumuika na wakazi wa maeneo ya Roysambu na Githurai. Kila mkenya ako na haki ya kuishi na kufanya kazi mahali popote nchini. HII KENYA NI YETU SISI SOTE.
> *We will not relent on our resolve to build a peaceful and stable Country. Wanainchi wameamua na kusema kwa kauli moja*: WEKA KWA KATIBA! (Hatutachoka na azimio letu la kujenga nchi dhabiti na yenye amani. Wananchi wameamua na kusema kwa kauli moja: WEKA KWA KATIBA!)

Kauli za washiriki

> 224. EK: Ndio baba usitishwe na mawe wala wheelbarrow kwani uliyapitia mengi, rege itambe baba.

Kauli hii inakiuka kipengele cha kanuni ya kiasi kinachomhitaji mzungumzaji kutoa habari zote muhimu zinazohitajika na msikilizaji ili kuelewa ujumbe kamili uliopo katika kauli fulani. Katika kauli hii, mshiriki EK anamweleza mhe. Odinga kuwa asitishwe na mawe wala wheelbarrow kwa sababu aliyapitia mengi. EK anakiuka kanuni ya kiasi kwa kutoa habari chache kuhusu ni mambo yepi mhe. Odinga aliyapitia. Kauli hii inamwacha msikilizaji na maswali kuhusu mambo au matatizo ambayo mhe. Odinga aliyapitia.

> Kauli ya 179. MGK: Aki baba wewe hunijenga najua mlima lazima utapanda wapende wasipende.
>
> Miitiko
>
> PK: Baba hatawahi kuwa prezo.
>
> MGK: **PK, Namm ningependa kukuambia ukon wana moba xnaaa. Baba prezo 2022. Mbona kuongea kaa mwenye Amekunywa *alcohol*.**

Kauli hii inahusisha mjadala kati ya washiriki wawili; MGK na PK. Katika kauli yake, MGK anamweleza mhe. Odinga kuwa anamfaa mbali na kumhakikishia kuwa angeenda mlima Kenya

wengine wapende au wasipende. Hali hii ilimfanya PK kumweleza kuwa mhe. Odinga hangewahi kuwa rais. MGK aliitikia kauli hii kwa kumweleza PK kuwa ana watoto wengi sana mbali na kuwa mhe. Odinga angekuwa rais 2022. Mshiriki huyu aliongeza kuwa PK alikuwa akiongea kama aliyekunywa pombe. Kauli hii inakiuka kipengele cha kutotoa habari nyingi zaidi ya zinazohitajika cha kanuni ya kiasi. MGK anamwitikia PK kwa kumweleza kuwa ana watoto wengi mbali na kuwa PK alikuwa akiongea kama aliyekunywa pombe. Hizi ni habari za ziada zisizohitajika katika kauli ya mzungumzaji.

Kauli ya 157. HKK: Watu wa githu walifunga biashara zao ili wakuone vile wanakupenda enyewe unapendwa sana central.

Mwitiko

MN: **Tuliongopa wizi ya mali yetu githurai tulijua anakuja na wakora kama kawaida hawachangi kibada ya mtu kama imesimama uliza wanabiashara wezangu watakupea story vizuri.**

Kauli hii inahusisha mjadala kati ya washiriki wawili ambao wanajadili ziara ya mhe. Odinga katika eneo la Githurai. Kulingana na HKK, watu wa Githurai walifunga biashara zao ili wamwone mhe. Odinga kwa sababu anapendwa sana katika mlima Kenya. Hata hivyo, MN anatofautiana na HKK kwa kumweleza kuwa walifunga biashara zao kwa sababu waliogopa mali zao zingeibwa kwa kuwa mhe. Odinga angekuja na 'wakora' wake ambao kulingana naye huharibu vibanda vya watu. Mshiriki huyu aliendelea na kauli yake kwa kumweleza HKK kuwa kama hamwamini, basi angewauliza wafanyabiashara wenzake ambao wangempa habari kamili. Kauli hii ya MN inakiuka kipengele cha kanuni ya kiasi kinachomhitaji mzungumzaji kutotoa habari nyingi zisizohitajika katika mazungumzo.

MN anamweleza HKK kuwa walijua mhe. Odinga angeenda katika eneo hilo na 'wakora' wake ambao huharibu vibanda vya wafanyibiashara. MN anaendelea kumwambia HKK kuwa kama hamwamini awaulize wafanyabiashara wengine ambao wangempaa habari kamili. Habari hizi si muhimu kwa mjadala unoendelea hivyo kuwa za ziada. Huu ni ukiukaji wa kanuni ya kiasi.

Kauli ya 7. DK: Na venye umepigwa githurai alafu unakuja kujigamba aty ulikuwa huku…

Mwitiko

AAA**: DK, wacha kudanganya watu ni wale machokora walikua Burma karibu 15 lakini wameona cha mtema kuni**.

Katika kauli hii, mshiriki AAA anapinga kauli iliyotolewa na DK kuwa mhe. Odinga alipigwa katika eneo la Githurai. Kulingana na AAA, DK hasemi ukweli kwa sababu walioleta vurugu katika eneo hilo walikuwa watoto wa mitaani 15 waliotoka Burma. Mshiriki huyu anaongeza kuwa watoto hao waliona cha mtema kuni. Hata hivyo, AAA haelezi kitu ambacho watoto hawa walifanyiwa ndiposa wakona cha mtema kuni. Mshiriki huyu basi ametoa habari chache kuhusu kilichowafanya watoto hao wakaona cha mtema kuni, hali ambayo inamwacha msikilizaji na maswali mengi ya kuuliza. Kauli hii basi inakiuka kipengele cha kanuni ya kiasi cha kutotota habari chache katika mazungumzo.

225. JO: Sawa baba, but nasikia ety oh mara ohh, ni ukweli?

Katika kauli hii, JO anamweleza mhe. Odinga kuwa kuna mambo anayoyasikia. Hata hivyo, JO anakosa kueleza ni mambo yepi anayoyasikia. Kauli yake haijaeleza habari zote zinazohitajika na msikilizaji ili kuweza kuelewa ujumbe unaowasilishwa. Kauli yake basi inakiuka kanuni ya kiasi.

Sasisho ya 2 (Februari 23/ 2021)

(*Sasisho hii ilitolewa na mhe. Odinga baada ya mabunge ya kaunti kupitisha mswada wa kubadilisha katiba wa BBI. Hali hii iliwapa washiriki katika mtandao wake wa Facebook kutoa maoni yao kuhusu kupitishwa kwa mswada huo wa BBI.* )

> *County assemblies have been able to push back on a year -long campaign of lies, misinformation and undue influence on a document whose Centre piece is ensuring prosperity and equitable sharing of the same.*
> *I thank the member of those county assemblies and our governors who refused to give in to mistrust, cynicism, brinkmanship and fear mongering and passed the bill resoundingly.*
> *As I said during the launch of the collection of signatures on the Bill, I have worked with our people on processes of change like this for a long time. I know for a fact that Kenyans are not slow learners when it comes to recognizing and seizing moments of change.*
> *That faith stands reaffirmed and renewed.*
> *With the dramatic and strong conclusion of the exercise today, we are extremely close to giving our people the reforms they need to create a united, inclusive, stable and prosperous nation that also deals decisively with the crime of corruption. I now look forward to working with our two houses of parliament.* (Mabunge ya kaunti yameweza kuondoa kampeni za uwongo, habari potovu na ushawishi mbaya kuhusu makala ambayo lengo lake ni kuhakikisha mafanikio na ugavi sawa. Nawashukuru wawakilishi wadi na magavana wetu ambao walikataa kukubali shaka, kiburi, uchovu na hofu na wakapitisha mswada huo.
> Kama nilivyosema wakati wa uzinduzi wa ukusanyaji wa saini za mswada huo, nimefanya kazi na wakenya katika mchakato wa mabadiliko kama huu kwa muda mrefu. Nina uhakika kuwa wakenya sio wagumu katika kufahamu mambo hususan katika kutambua na kukumbatia nyakati za mabadiliko.
> Imani hii imethibitishwa na kuzinduliwa upya.
> Kuhitimishwa kwa shughuli hii leo kunaashiria kuwa tuko karibu kuwapa wakenya mabadiliko wanayotaka ili kujenga nchi yenye umoja, imara na yenye mafanikio ambayo pia inatatua shida ya ufisadi. Nalenga sasa kufanya kazi na mabunge yetu mawili.)

Kauli za washiriki

Kauli ya 10. GCK: Ujinga tu…mujinga ya mtu, …ni sawa tu, tunaelewa shida ya uzee.

Katika kauli hii, mshiriki GCK anatumia kauli yenye utopole kuhasiri uso wa mhe. Odinga. Katika kauli yake, GCK anamweleza mhe. Odinga kuwa wanaelewa shida ya uzee. Mshiriki huyu hajaeleza shida ya uzee inahusu nini, hali ambayo inamwacha msikilizaji na maswali ya kuuliza kuhusu nini hasa shida ya uzee kama anavyoeleza GCK. Kauli hii basi inakiuka kanuni ya kiasi kwa kutoa habari chache ambazo zinaufanya ujumbe uliowasilishwa na mzungumzaji kutoeleweka vizuri.

> Kauli ya 134. CG: kwa ground mtatupata mjue hamjatuhonga, mkumbuke after Judas kumasaliti yesu kwa zile pesa alikula hongo baadaye akajinyonga, uzuri Mungu anamuona nyinyi mtetezi wa wanjiku ni mungu tu.

Katika kauli hii, mshiriki CG anaitikia hali ya madiwani kupitisha mswada wa BBI ambapo anaeleza kuwa waliopitisha mswada huo wangewapata mashinani kwa debe kwa kuwa hawakuwahonga. Mshiriki anaendelea na kauli yake kwa kuwaeleza kuwa wanafaa kukumbuka kujinyonga kwa Judas baada ya kumsaliti Yesu kwa sababu ya pesa. Mshiriki huyu anahitimisha kauli yake kwa kuwatisha walengwa wake kuwa Mungu anawaona mbali na kuwa mtetezi wa mwananchi wa kawaida. Mshiriki huyu ameondoka nje ya mada ya mazungumzo na kuzungumzia masuala ya kujinyonga kwa Judas kwa sababu ya pesa na hata kuwatisha wasikilizaji wake. Kupitia habari hizi, CG anakiuka kanuni ya kiasi kwa kutoa habari nyingi zaidi zisizohitajika katika mazungumzo.

> Kauli ya 14. AM: …leteni iyo bibi yai kwa wananchi tutaiangusha…kumbuka uyo kijana mlevi alikua anasema kimundu bado utaremain kuwa kimundu.

Mshiriki AM anamweleza mhe. Odinga kuwa wangeangusha mswada wa BBI kama wangeupeleka kwao mashinani. Mshiriki huyu anaendelea na kauli yake kuwa mhe. Kenyataa alikuwa akimwita mhe. Odinga kwa jina ‘kimundu’ na kuwa hali hiyo haingebadilika. Mshiriki huyu anakiuka kanuni ya kiasi kwa kuzungumzia habari isiyo na umuhimu kwa mada inayozungumziwa anapoingiza habari kuhusu jina ambalo mhe. Kenyatta alikuwa akitumia kumrejelea mhe. Odinga. Hii ni habari ya ziada isiyohitajika katika mjadala huu.

> Kauli ya 15. JN:…Tunangoja hiyo REFERENDUM tupitishe na hakuna kitu Ruto atafanya.

Katika kauli hii, mshiriki huyu anakiuka kanuni ya kiasi kwa kutoa habari nyingi zisizohitajika katika mazungumzo. Kulingana na JN, wanangoja kura ya maamuzi ili kupitisha mswada wa BBI. Ukiukaji wa kanuni ya kiasi unatokea wakati mshiriki huyu anamwingiza mhe. Ruto katika kauli yake kwa kueleza kuwa hakuna kitu chochote angefanya ili kuzuia upitishaji wa mswada huo. JN basi anashirikisha habari ya ziada katika kauli yake isiyo muhimu kwa mada ya mazungumzo.

> Kauli ya 152. KM: Haina shida kichapo ni kile kimoja…wembe ni ule tu.

KM anamtisha mhe. Odinga kwa kumweleza kuwa kichapo ni kile kimoja na wembe ni ule tu. Mshiriki huyu hajaeleza aina ya kichapo ambacho kinahusika wala wembe waliotumia. Kauli yake inamwacha msikilizaji wake na maswali mengi kuhusu aina ya kichapo kinachohusika. Kauli hii basi kinakiuka kanuni ya kiasi kwa sababu imetoa habari chache kuliko zinazohitajika.

> 226. OJ: BBI ikipita petrol itakua 1lit@200/= mtanikumbuka kwa hilo na hakuna mshahara utaongezwa kwa mwananchi wa kawaida.

Katika kauli hii, mshiriki OJ anawaonya watu kuwa endapo mswada wa BBI ungepita, basi lita moja ya petrol ingeuzwa kwa shilingi 200. Mshiriki huyu anaendelea na kauli yake kwa kuongeza kuwa watu wangemkumbuka kwa onyo hilo mbali na kuwaeleza kuwa hakuna mshahara ambao wangeongezwa. Kauli hii inakiuka kanuni ya kiasi kwa kuwa inahusisha habari nyingi zisizohitajika. Habari za kukumbukwa kwa onyo alilotoa na kutoongezwa kwa mshahara kwa wananchi wa kawaida si muhimu kwa kuwa hazihusiani na mada ya mazungumzo.

> Kauli ya 17. NWKW: Nyamazisha mdomo sema mliwablibe naukatumia uganga wako!!!...ata shetani aombe mungu msamaha huwezi kuwa president wa Kenya.

Mshiriki NWKW anamweleza mhe. Odinga kuwa yeye pamoja na wenzake waliwahonga madiwani mbali na kutumia uganga wake ili kuhakikisha kuwa mswada wa BBI ulipitishwa. Hata hivyo, mshiriki huyu anaongeza kuwa mhe. Odinga hawezi kuwa rais wa Kenya hata kama shetani angemwomba Mungu msamaha. Habari hii si muhimu kwa mada ya mazungumzo mbali na kutohusiana na mada hiyo. Kupitia habari hii, kauli hii basi inakiuka kanuni ya kiasi kwa kuwa inakiuka kipengele kinanchomhitaji mzungumzaji kutotoa habari nyingi zisizo muhimu.

> Kauli ya 100. SO: Kwenda uko Uhuru alipeana pesa, wewe unafurahia nurse wakikosa pesa Lakini ukue president.

Katika kauli hii, SO anatofautiana na mhe. Odinga kuhusu namna mswada wa BBI ulipitishwa na madiwani. Kulingana na SO, mswada huo ulipitishwa kwa sababu mhe. Kenyatta aliwapa madiwani hao pesa. Kando na habari hii, SO anaongeza kuwa mhe. Odinga anafurahi wakati wauguzi wanakosa pesa mradi awe rais. Kufurahi kwa mhe. Odinga na kukosa pesa kwa wauguzi ni habari ambazo si muhimu kwa mada ya mazungumzo. Habari hizi ni za ziada hivyo zinakiuka kanuni ya kiasi ambayo inamhitaji mzungumzaji kutoa habari muhimu zinazohitajika tu.

> Kauli ya 139. BG: Hii kiti umeitafuta xana mzee. Mungu anakuona vile unahangaisha wakenya

Mshiriki BG anamweleza mhe. Odinga kuwa amekitafuta sana kiti fulani kando na kuwahangaisha wakenya. Mshiriki huyu hajaeleza ni kiti gani haswa ambacho mhe. Odinga amekitafuta sana mbali na kutoeleza jinsi mhe. Odinga huhangaisha wakenya. BG basi anakiuka kanuni ya kiasi kwa kutoa habari chache ambazo zinamwacha msikilizaji wake na maswali mengi kuhusu kiti kilichotafutwa na pia jinsi wakenya huhangaishwa.

Kauli ya 165. SSS: Eti baba amekubali matokeo?

Katika kauli hii, SSS anauliza iwapo mhe. Odinga alikubali matokeo. Hata hivyo, kauli yake haijaeleza ni matokeo yepi ambayo mhe. Odinga alifaa kuyakubali. Kauli hii basi inamwacha msikilizaji na maswali ya kujiuliza kuhusu aina ya matokeo husika. Hivyo, SSS anakiuka kanuni ya kiasi kwa kutoa habari chache zaidi ya zinazohitajika katika muktadha wa mazungumzo.

Kauli ya 167. KM: Kuna wakati pia mm nilicheat kwa cut nikawa number one wacha KCSE ifike.

KM anaeleza kuwa kuna wakati aliwahi kudanganya katika mtihani shuleni na akawa wa kwanza. Hata hivyo, mshiriki huyu hajaeleza kilichofanyika baada ya kufanya mtihani wa kitaifa wa KCSE. Kutoeleza habari hii kunamfanya ujumbe wake usieleweka vizuri. Msikilizaji wake basi anawachwa na maswali ya kujiuliza kuhusu kilichotokea baada ya mzungumzaji kufanya mtihani huo. Kauli ya KM basi inakiuka kanuni ya kiasi kwa kutoa habari chache kuliko zinazohitajika.

227. SO: MAMA NI MCHAWI, BABA MALAYA MTOTO NI

Katika mfano huu, SO anatoa kauli isiyohusiana na mada ya mazungumzo. Mshiriki huyu anatoa kauli ambayo haijakamilika na ambayo inamwacha msikilizaji wake kutaka kujua mtoto anayerejelewa ni nini. Kauli yake basi inakiuka kanuni ya kiasi kwa kutoa habari chache kuliko zinazohitajika.

Kauli ya 50. JD: Hakuna mwanaume mwizi kama raila. Huwa uko na sura mbaya na bado unaibia Kenyans. Constitution na bbi zimesaidia nani ka si nyinyi pekee. Sina ubaya nikikuita jambazi.

Katika kauli hii, mshiriki JD anakiuka kanuni ya kiasi kwa kutoa habari nyingi zisizohitajika. Mbali na kumweleza mhe. Odinga kuwa yeye ni mwizi na kuwa ana sura mbaya, JD anamrejelea mhe. Odinga kwa kitambulisho kisichofaa 'jambazi'. Hizi ni habari zisizo muhimu kwa mada inayozungumziwa ambayo ni kupita kwa mswada wa BBI. JD basi ameshirikisha habari nyingi ambazo zinafanya kauli yake kutoeleweka vizuri. Pia, JD anakiuka kanuni ya kiasi kwa kutumia neno 'mwanaume' kumrejelea mhe. Raila. Hakuna haja ya kutumia neno 'mwanaume' kwa sababu inajulikana kuwa jinsia ya mhe. Odinga ni ya kiume. Hivyo, JD amekiuka kanuni ya kiasi kwa kurudia habari fulani.

Kauli ya 71. PKL: Wewe ni mtu hana akili, wewe tunakusupport pale tunajua hautafaidika na kitu…wewe ni mtu wa mkono wa Uhuru.

PKL anamweleza mhe. Odinga kuwa hana akili kwa kuwa wanamuunga mikono pale ambapo hawezi kufaidika. Mshiriki huyu anaongeza kuwa mhe. Odinga ni mtu wa mkono wa rais Kenyatta. Kauli ya PKL inahusisha habari nyingi zisizo muhimu kwa mada ya mazungumzo.

Habari hizi inamfanya msikilizaji wake kuwa na ugumu katika kuelewa ujumbe uliopo. Mshiriki huyu basi anakiuka kanuni ya kiasi kwa kutoa habari nyingi zisizohitajika katika muktadha husika wa mazungumzo.

Kauli ya 52. JM: Mganga lipa deni ya Kalonzo Musyoka na Mudavadi kwanza.

Katika kauli hii, JM anamweleza mhe. Odinga kulipa deni la mhe. Kalonzo Musyoka na mhe. Mudavadi kabala kuzungumzia mswada wa BBI. Hata hivyo, mshiriki huyu amekosa kutaja ni deni aina gani ambalo mhe. Odinga anafaa kuwalipa wanasiasa hawa. Kauli hii basi inakiuka kanuni ya kiasi kwa kutoa habari chache ambazo zinamfanya msikilizaji kuwa na maswali, hivyo kutoelewa kikamilifu ujumbe unaowasilishwa.

228. JMW: Leo utalala na viatu.

Mshiriki huyu anamweleza mhe. Odinga kuwa angelala akiwa amevaa viatu. Kauli yake hata hivyo haijaeleza ni kwa nini mhe. Odinga angelala akiwa amevaa viatu. Sababu ya JMW kutoa kauli hii haijaelezwa. Kauli hii basi imeshirikisha habari chache ambazo zinaufanya ujumbe wa JMW kutoeleweka vizuri. Hali hii inakiuka kanuni ya kiasi inayomhitaji mzungumzaji kutotoa habari chache zisizoeleweka.

229. OVA: Baba siwezi lala leo.

Katika kauli hii, OVA anamweleza mhe. Odinga kuwa hangeweza kulala siku hiyo. Mzungumzaji huyu hata hivyo hajaeleza sababu za kutolala kwake. Kauli hii basi inashirikisha habari chache ambazo zinamfanya msikilizaji kuwa na maswali ya kujiuliza kuhusu kauli iliyotolewa. Kauli hii inakiuka kipengele cha kanuni ya kiasi kinachomhitaji mzungumzaji kutotoa habari chache katika mawasiliano.

Sasisho ya 3 (Machi 11, 2021)

(*Sasisho hii ilitolewa na mhe. Ruto ambaye wakati huu alikuwa naibu wa rais wa Kenya na ambaye alichukuliwa kuwa angekuwa mpinzani mkuu wa mhe. Odinga katika uchaguzi wa mwaka wa 2022. Katika kiungo hiki, mhe.Ruto alitumia ukurasa wake wa Facebook kumtakia heri na hali ya nafuu mhe. Odinga ambaye wakati huu alikuwa mgonjwa kutokana na virusi vya UVIKO 19. Hatua hii iliwashangaza watu wengi wakiwemo wafuasi wake wa kisiasa na hata wale wa mhe. Odinga ambao walimuona kama aliyekuwa akimkejeli mhe. Odinga. Wengi waliweza kutoa maoni yao kuhusu hatua hii*.)

> *To Raila Odinga, former PM, Isaih 53v5 by Jesus stripes comes healing. You have fought many battles, you have always demonstrated courage and bravery. This too you will overcome. Quick recovery my friend. The nation is praying.* (Kwa Raila Odinga, aliyekuwa waziri mkuuu, Isaya 53v5 kwa kupigwa kwake Yesu tumepona. Umepitia changamoto nyingi, na umeweza kudhihirisha ujasiri na ushujaa. Hii pia utashinda. Pona haraka rafiki yangu. Taifa linaomba.)

Kauli za washiriki

Kauli ya 144. KK: Apone haraka akuje tena atutusi vile amezoea, tutamweka kwa wheelbarrow tumpeleka lake Victoria.

Katika kauli hii, KK anakiuka kanuni ya kiasi kwa kutoa habari nyingi zaidi ya zinazohitajika. Mshiriki huyu anamtakia heri mhe. Odinga baada ya kuugua kutokana na virusi vya corona. Habari za ziada zinahusu kauli za KK kuwa kuwa wanamngoja aje awatusi tena kama alivyozoea mbali na kumtisha kuwa wangemweka kwa wheelbarrow hadi ziwa Victoria. Habari hizi si muhumu kwa mada inayohusika, hivyo hazihitajiki na msikilizaji.

Kauli ya 55. EE: Aliiba pesa ya corona na vinyangarika wake. Alidhani anaeza hepa.

Katika kauli hii, EE anaeleza kuwa mhe. Odinga pamoja na wenzake walihusika katika kuiba pesa zilizotengewa virusi vya corona. EE anaongeza kwa kusema kuwa mhe. Odinga alidhani angehepa. Kauli yake haijaeleza kwa kikamilifu kitu au hali ambayo mhe. Odinga alifikiria anaweza kuhepa. Hali hii basi inamfanya msikilizaji wake kutoelewa ujumbe wake kikamilifu kwa kuwa habari alizozitoa ni chache kuliko zinazohitajika na msikilizaji. Kauli hii inakiuka kanuni ya kiasi.

Sasisho ya 4 (Machi, 12 2021)

(*Sasisho hii ilitolewa na mhe. Ruto baada ya rais wa wakati huo nchini Kenya mhe. Uhuru Kenyatta kutangaza kuwa mikutano yote ya kisiasa ilipigwa marufuku kutokana na kuongezeka kwa idadi ya maambukizi ya virusi vya Corona nchini. Kutokana na hali hii, mhe. Ruto alienda katika ukurasa wake wa Facebook ili kuwajulisha wafuasi wake kuwa ameahirisha mikutano yake yote ya kisiasa.)*

*The COVID 19 infection rates have become a serious source of concern making it necessary for GOK to take remedial measures to manage and contain the pandemic. With the president's announcement of containment measures, I forthwith suspend all public engagements until further notice.* (Idadi ya maambukizi ya virusi vya UVIKOA 19 imekuwa changamoto kubwa hivyo kuifanya serikali ya Kenya kuchukua hatua za ziada ili kudhibiti janga hili. Kutokana na tangazo lililotolewa na rais kuhusu mikakati ya kudhibiti ugonjwa huu, nimeamua kuahirisha mikutano yangu yote ya hadhara.)

Kauli za washiriki

Kauli ya 154. MJ: President amesema jaribu uone!!! Kwa hvo ni uoga uko nayo vile prezzo ametisha.

Katika kauli hii, MJ ameitikia sasisho iliyoandikwa na mhe. Ruto kwa kumweleza kuwa rais ametoa amri ambayo hawezi kukiuka. MJ alikiuka kanuni ya kiasi kwa kuongeza katika kauli yake kuwa mhe. Ruto hawezi kwenda kinyume na amri ya rais kwa sababu ya uwoga alionao.

Hii ni habari ambayo si muhimu kwa msikilizaji kwa kuwa haihusiani na mada ya mazungumzo. Kauli hii basi inakiuka kipengele cha kanuni ya kiasi kinachomhitaji mzungumzaji kutotoa habari nyingi zaidi ya zinazohitajika.

> Kauli ya 33. PC: Hii lazima utii…Ouru na Odinga washaamua ingia sugoi na ulimelime kiasi.

Kauli ya PC inakiuka kanuni ya kiasi kwa kutoa habari nyingi zisizohitajika. Mshiriki huyu anamweleza mhe. Ruto kuwa lazima angetii amri iliyotolewa na rais. Hata hivyo, ukiukaji wake wa kanuni ya kiasi unadhihirika anapoeleza kuwa mhe. Uhuru na Odinga washaamua hivyo analoweza kufanya mhe. Ruto ni kwenda Sugoi ili aanze shughuli ya kulima. Hizi ni habari za ziadi zisizo muhimu kwa mada husika.

> Kauli ya 145. GBM: Tulia umesambaza kwa wingi.

Katika kauli hii, GBM anamweleza mhe. Ruto kuwa atulie kwa sababu amesambaza kwa wingi. Hata hivyo, mshiriki huyu hajaeleza nini mhe. Ruto amesambaza kwa wingi, hali ambayo inaufanya ujumbe katika kauli yake usieleweke vizuri. Kauli hii basi inahusisha habari chache kuliko zinazohitajika na msikilizaji.

<u>Sasisho ya 5 (Aprili, 22, 2021)</u>
*(Sasisho hii ilitolewa na mhe. Ruto baada ya kukutana na aliyekuwa gavana wa banki kuu ya Kenya, profesa Njuguna Ndung'u. )*

> *The state of the global economy demands new thinking, bold ideas and fresh paradigms. We must include more Kenyans in the growth of our country. This is why we are proposing a bottom-up approach to develop the economy.*
> *This approach will ensure more resources are invested in the grassroots, greater economic participation and an expansion of the tax base.*
> *It is gratifying to see economic experts endorsing this approach and expressing willingness to partner with us to actualize this revolution.*
> (Hali ya uchumi duniani inahitaji fikra mpya, mawazo komavu na mwanzo mpya. Lazima tuwashirikishe wakenya wengi katika kujenga nchi yetu. Hii ndiyo sababu tunapendekeza ukuaji wa uchumi kupitia mfumo wa kutoka chini kwenda juu.
> Mfumo huu utahakikisha kuwa rasilimali zimewekezwa mashinani, ushiriki wa kutosha katika masula ya kiuchumi na upanuzi wa viwango vya ushuru.
> Ni furaha kuwaona wanauchumi wakiuunga mikono mfumo huu mbali na kuonyesha azma yao ya kuungana nasi ili kuzalisha hali hii.)

<u>Kauli ya mshiriki</u>
> 230. DA: Hii shati ya Ruto inakaa ile ya msalaba ya independent church..ama ni njaa inanisumbua.

DA ameitikia sasisho iliyotolewa na mhe. Ruto kwa kuzungumzia shati alilovaa na kulilinganisha na msalaba unaotumiwa na kanisa la Independent. Ukiukaji wake wa kanuni ya kiasi unadhihirika anapoeleza kuwa huenda ni njaa inamsumbua. Hii ni habari ya ziada isiyo muhimu kwa mada husika. Kupitia habari hii ya ziada, kipengele cha kanuni ya kaisi kinachomhitaji mzungumzaji kutotoa habari nyingi zisizohitajika kinakiukwa na DA.

**6.2 Ukiukaji wa Kanuni ya Uhusiano**

Kanuni ya uhusiano hukiukwa ikiwa mzungumzaji atatoa kauli au maoni yasihohusiana na mada ya mazungumzo. Kanuni hii hukiukwa ikiwa mzungumzaji atazungumzia mada iliyo nje ya mada ya mazungumzo. Kulingana na Grice (1975), kanuni ya uhusiano hukiukwa ikiwa mzungumzaji atazungumzia hoja isiyohusiana na mada ya mazungumzo, mzungumzaji kugeuza mada ya mazungumzo ghafla, mzungumzaji kukosa kuzungumzia hoja fulani na ikiwa mzungumzaji atasababisha matokeo hasi kutokea. Kupitia vipengele hivi, mtafiti aliweza kukusanya kauli ambazo zilikiuka kanuni hii. Utafiti ilibainisha kuwa washiriki wengi wa mtandao wa *Facebook* hutoa kauli nyingi zilizo nje ya mada ya mazungumzo ili kueleza hoja zao. Ukiukaji wa kanuni hii ulijitokeza kwa njia zifuatazo:

<u>Sasisho ya 1</u>

(*Muktadha wa mazungumzo: Kauli hizi zilitolewa na washiriki baada ya sasisho iliyotolewa na mhe. Odinga baada ya kuzuru eneo la Githurai ambapo alieleza kuwa alifurahi kuzuru na kujumuika na wakazi wa Roysambu na Githurai mbali na kuwa kila mkenya alikuwa na haki ya kuishi na kufanya kazi mahali popote nchini.*)

> Kauli ya 1. MM: Kama kawaida tutaamka asubuhi na mapema 2022 kuhakikisha hujakanyaga ikulu.

Katika kauli hii, mshiriki MM aliitikia sasisho ya mhe. Odinga kwa kumweleza kuwa kama kawaida yao, wangeamka asubuhi na mapema mwaka wa 2022 ili kuhakikisha hajakuwa rais. Kauli ya MM haijahusiana na mada husika ya mazungumzo. Kauli hii basi inakiuka kanuni ya uhusiano kupitia kipengele cha mzungumzaji kutoa hoja isiyohusiana na mada ya mazungumzo.

> 231. LW: Tumekuja tumeshangilia lakini hii story ya watu wa kariobangi kulala nje itawaangusha na ndugu yako.

Katika mfano huu, LW anakiuka kanuni ya uhusiano kwa kugeuza mada ya mazungumzo ghafla. Hali hii inatokea pale ambapo LW anaanza kwa kuzungumzia ziara ya mhe. Odinga kule Githurai na baadaye kighafla, anageuza mada ya mazungumzo na kuanza kuzungumzia shida inayowakumba watu wa Kariobangi. Kugeuza mada ya mazungumzo ghafla ni ukiukaji wa kanuni ya uhusiano.

> 232. DN: nimefukuzwa shule juu ya fees n saidie.

Katika kauli hii, DN anakiuka kanuni ya uhusiano kwa kuzungumzia hoja isiyohusiana na mada

ya mazungumzo. Katika kauli yake, DN anazungumzia hoja ya kukosa karo ya shule hali inayomfanya kuomba msaada. Kauli hii haihusiani na mada ya mazungumzo inayojitokeza katika sasisho iliyowasilishwa na mhe. Odinga.

233. CA: Kapedo na Mandera county si Kenya.

CA anakiuka kanuni ya uhusiano kwa kuzungumzia hoja isiyohusiana na mada ya mazungumzo. Mzungumzaji huyu badala ya kuzungumzia ziara ya mhe. Odinga katika eneo la Githurai, anazungumzia suala la Kapedo na kaunti ya Mandera kuwa si sehemu ya Kenya. Kauli yake haihusiani kwa njia yoyote na mada iliyowasilishwa na mhe. Odinga.

<u>Sasisho ya 2</u>

(*Muktadha wa mazungumzo: Kauli hizi zilitolewa na washiriki wa mtandao wa Facebook kama njia ya kuitikia sasisho iliyotolewa na mhe. Odinga baada ya mabunge ya kaunti kupitisha mswada wa BBI. Katika sasisho hiyo, mhe. Odinga alionyesha imani yake kwa madiwani mbali na kutaka mabunge ya seneti na la kitaifa kuidhinisha mswada huo.*)

Kauli ya 8. SM: Uzuri debe tutaiangusha..
Miitiko
BO: SM, unafikiria hiyo debe wewe pekeako ndo utapiga kura? #senji
Kauli ya 207. SM: **BO, wewe ndo utapiga peke yako pia?**
KJR: SM, hiyo debe inahesabiwa na serikali bado sio wanjiku.
GA: KJR, …nakuhurumia.
KJR: GA, sasa kati yangu na yako nani anafaa kuhurumia mwingine?
Kauli ya 208. **GA: KJR, siezi ulizwa swali ilikuwa jibu…**

Katika kauli ya 207, mshiriki SM anakiuka kanuni ya uhusiano kwa kutojibu swali aliloulizwa na BO na badala yake kumuuliza kama yeye ndiye atapiga kura peke yake. Msikilizaji wake ambaye ni BO, alimtarajia amjibu kama yeye peke yake ndiye atapiga kura au la. Mzungumzaji huyu ametumia kipengele cha kutozungumzia hoja fulani ili kukiuka kanuni ya uhusiano. Sawa na SM, katika kauli ya 208, mshiriki GA naye anakosa kujibu swali aliloulizwa na KJR kuhusu ni nani kati yao anafaa kumhurumia mwingine. Badala ya kujibu swali hili, GA anapuuza swali lake na kumwambia kuwa hawezi kuulizwa swali ambalo ni jibu. Hili si jibu ambalo KJR alitarajia kutoka kwa GA. Kupitia kauli hii, mshiriki huyu anakiuka kanuni ya uhusiano.

Kauli ya 9. DAI: Wewe utaona kiti cha urais kwa viusasa.

Katika kauli hii, DAI anakiuka kanuni ya uhusiano kwa kuzungumzia hoja isiyohusiana na mada ya mazungumzo. Mshiriki huyu badala ya kuzungumzia mada iliyowasilishwa na mhe. Odinga kuhusu ziara yake katika eneo la Githurai, anazungumzia uwezo wa mhe. Odinga kuwa rais wa Kenya. Suala hili halihusiani na mada ya mazungumzo.

Kauli ya 44. CW: Wale mnaitanga uyu mganga baba hamjui baba zenu ama mama zenu waliwaambia uyu ndio baba yako!!!

Katika kauli hii, mshiriki CW anakiuka kanuni ya uhusiano kwa kuzungumzia hoja isiyohusiana na mada ya mazungumzo. CW anazungumzia kitambulisho ambacho wafuasi wa mhe. Odinga hutumia kumrejelea. Hoja zinazobainika katika kauli hii hazihusiani na ujumbe uliopo kwenye mada ya mazungumzo.

Kauli ya 165. SSS: Eti baba amekubali matokeo?
Mwitiko
AN: **SSS, Dio nashangaa…**

Katika mfano huu, AN anakiuka kanuni ya uhusiano kwa kukosa kujibu swali liloulizwa na SSS. Mhiriki SSS aliuliza iwapo mhe. Odinga alikubali matokeo. Mshiriki huyu alitarajia jibu la ndio au la ila AN aliitikia kauli hiyo kwa kutoa kauli isiyojibu swali husika. AN basi anakiuka kanuni ya uhusiano kwa kutozungumzia hoja husika.

Kauli ya 139. BG: Hii kiti umeitafuta xana mzee. Mungu anakuona vile unahangaisha wakenya.

Katika mfano huu, mshiriki BG anakiuka kanuni ya uhusiano kwa kuzungumzia hoja isiyohusiana na mada ya mazungumzo. BG anazungumzia namna mhe. Odinga alivyotafuta kiti cha urais mbali na kueleza kuwa anazidi kuwahangaisha wakenya. Hizi ni habari zisizohusiana na mada ya mazungumzo ambayo ni kupitishwa kwa mswada wa BBI na mabunge ya kaunti.

Kauli ya 140. JK: …utakaposhindwa wakati wa uchaguzi mkuu, usilete kasheshe, sokomoko, vitimbi na mvurugano. Ukumbali umedhidwa na uelekee nyumbani.

Katika kauli hii, JK anakiuka kanuni ya uhusiano kwa kuzungumzia hoja isiyohusiana na mada ya mazungumzo. JK anamweleza mhe. Odinga kuwa ikiwa atashindwa katika uchaguzi mkuu, asilete kasheshe na vurumai na badala yake akubali na kisha kwenda nyumbani. Habari zilizoko kwenye kauli hii hazihusiani na ujumbe uliowasilishwa na mhe. Odinga. Kauli hii haihusiani na kupitishwa kwa mswada wa BBI.

Kauli ya 52. JM: Mganga lipa deni ya Kalonzo Musyoka na Mudavadi kwanza.

Kauli ya JM inakiuka kanuni ya uhusiano kwa kuwa inazungumzia hoja isiyohusiana na mada ya mazungumzo. JM anazungumzia deni alilonalo mhe. Odinga ambalo anafaa kuwalipa wanasiasa mhe. Kalonzo na Mudavadi. Habari iliyopo kwenye kauli hii haihusiana na kupitishwa kwa mswada wa BBI na mabunge ya kaunti.

234. EO: Raila baba Fedel nilikuombea mola upone.

Katika kauli hii, EO anazungumzia jinsi alimwombea mhe. Odinga Mola ili aweze kupona. Kauli hii inakiuka kanuni ya uhusiano kwa kuwa EO anazungumzia hoja isiyohusiana na mada ya mazungumzo.

235. S: Ni lini utatupeleka Canaan?

Mshiriki S anamuuliza mhe. Odinga wakati gani angewapeleka Canaan. S amekosa kuzungumzia habari zilizoko kwenye mada ya mazungumzo. Hivyo, S amekiuka kipengele cha kanuni ya uhusiano kinachomhitaji mzungumzaji kutozungumzia hoja isiyohusiana na mada ya mazungumzo.

236. MI: Watu wa molo tuaze kuhama naona vita kubwa 2022.

Kauli ya MI inakiuka kipengele cha kanuni ya uhisiano kinachomhitaji mzungumzaji kutozungumzia hoja isiyohusiana na mada ya mazungumzo. MI anawaeleza wakaazi wa Molo kuwa wanafaa kuanza kuhama kwa sababu vita vikubwa vingetokea mwaka wa 2022. Hii ni hoja isiyohusiana na mada ya mazungumzo.

Sasisho ya 3

*(Muktadha wa mazungumzo: kauli hizi zilitolewa na washiriki wa mtandao wa Facebook kama njia ya kuitikia sasisho iliyotolewa na mhe. Ruto ambayo ilimtakia heri na hali ya nafuu mhe. Odinga ambaye alikuwa mgonjwa kutokana na virusi vya corona)*

Kauli ya 53. CKA: Najua kindani vile unawaza bwana kiambaa…
Miitiko
GG: Mseme ukweli, mnatamani afe.
237. AWC: **GG, kwani yeye ndiye atakuwa wa kwanza aaah…**
238. BOO**: CKA, ulitairi wewe kweri.**
MM: CKA, uyo hata akufe akuna kitu anasaidia Kenya.
PMM: MM, unataka akusaidie wewe
239. MM: **PMM, akufe, hakuna kubembelezwa hapa…puga.**

Katika kauli ya 237, mshiriki AWC anakiuka kanuni ya uhusiano kwa kutozungumzia hoja iliyowasilishwa na GG. AWC amekosa kueleza kama ni kweli wanatamani mhe. Odinga afe au la na badala yake anazungumzia hali ya mhe. Odinga kutokuwa wa kwanza kufa. Kauli ya 238 nayo inakiuka kanuni ya uhusiano kwa kubadilisha mada ya mazungumzo. BOO ameitikia kauli iliyotolewa na CKA kwa kumuuliza kama kweli alitahiriwa. Habari iliyopo penye kauli hii haihusiani na ujumbe uliopo penye kauli iliyowasilishwa na CKA. Mshiriki MM naye anakiuka kanuni ya uhusiano kwa kukosa kuzungumzia hoja iliyowasilishwa na PMM. PMM alimuuliza iwapo alimtaka mhe. Odinga amsaidie lakini MM aliitikia kauli hii kwa kueleza kuwa anafaa afe kwa kuwa hakuna kubembelezwa. Kauli hii haihusiani na ujumbe uliowasilishwa na kauli ya PMM.

Sasisho ya 4

(*Muktadha wa mazungumzo: Kauli hii ilitolewa na mshiriki wa mtandao wa Facebook kama njia ya kuitikia sasisho iliyotolewa na mhe. Ruto ambayo iliwaeleza wakenya kuhusu kusitisha kwake kwa mikutano yake ya kisiasa kwa sababu za kuongezeka kwa virusi vya corona nchini. Hali hii ilitokana na agizo lililotolewa na rais)*

240. PO. Tunamshukuru naibu rais kwa kutembelea mjini Busia tuko pamoja kwa kuchangia wanaichi wa chini.

Kauli hii inakiuka kanuni ya uhusiano kwa kuwa haihusiani na ujumbe uliowasilishwa katika sasisho iliyotolewa na mhe. Ruto. PO anamshukuru mhe. Ruto kutokana na matembezi aliyofanya katika eneo la Busia mbali na kuwachangia pesa wananchi wa kawaida. Ujumbe uliopo kwenye kauli hii hauhusiani na mada husika. Mshiriki huyu basi anakiuka kipengele cha kanuni ya uhusiano kinachomhitaji mzungumzaji kutozungumzia hoja isiyohusiana na mada ya mazungumzo.

Sasisho ya 5

(*Muktadha wa mazungumzo: kauli hizi zilitolewa na washiriki ili kuitikia sasisho iliyowasilishwa na mhe. Ruto kuhusu namna ya kufufua uchumi wa nchi kupitia mfumo wa kutoka chini hadi juu.)*

Kauli ya 173. OEM: iyo sharti ni msalaba ya kiambaa ama?

Katika mfano huu, OEM anazungumzia shati alilolivaa mhe. Ruto ambalo analifananisha na msalaba wa Kiambaa. Mshiriki huyu amekosa kuzungumzia hoja iliyowasilishwa na mhe. Ruto ambalo ni kufufua uchumi kwa kuwashirikisha wananchi wa kawaida. Huu ni ukiukaji wa kipengele cha kanuni ya uhusiano kinachomhitaji mzungumzaji kutozungumzia hoja isiyohusiana na mada ya mazungumzo.

Kauli ya 148. MKK: Unapanga kuiba wapi tena.

Katika kauli hii, MKK anamuuliza mhe. Ruto alikopanga kuiba tena. Kauli yake haihusiani na ujumbe uliowasilishwa na mhe. Ruto. Kanuni hii basi inakiukakipengele cha kanuni ya uhusiano kinachomhitaji mzungumzaji kutozungumzia hoja isiyohusiana na mada ya mazungumzo.

**6.3 Ukiukaji wa Kanuni ya Ukweli**

Hii ni kanuni inayomhitaji mzungumzaji kutoa kauli ambazo ni za kweli na zinazoweza kuthibitika. Katika kauli hii, mzungumzaji anahitajika kutoa kauli ambazo ana ushahidi wa kutosha. Ukiukaji wa kanuni ya ukweli hutokea ikiwa mzungumzaji atatoa kauli ambayo si kweli na ambayo hawezi kuthibitisha. Hali hii huweza kutokea kwa sababu mbalimbali kama vile mgongano wa kanuni za ushirikiano ambapo mzungumzaji analazimika kuzingatia kanuni fulani lakini akapuuza kanuni ya ukweli. Utafiti umebainisha kuwa hali hii hutokea katika diskosi ya siasa hususan washiriki wanapotaka kutoa maelezo kuhusu hali fulani au kuwasawiri wapinzani wao kwa njia hasi. Kulingana na Grice (1975), kanuni ya ukweli hukiukwa ikiwa mzungumzaji hatatoa kauli yenye ukweli, atatoa kauli yenye kejeli au kinaya, mzungumzaji

atakataa kauli fulani na ikiwa mzungumzaji atavunja habari husika. Kanuni hii imekiukwa kwa njia zifuatazo:

Sasisho ya 1

241. MGK: Aki baba wewe hunijenga najua mlima lazima utapanda wapende wasipende.

Mwitiko

PK: **Baba hatawai kuwa prezo. (Baba hatawahi kuwa rais.)**

Mwitiko uliotolewa na PK unakiuka kanuni ya ukweli kwa kuwa unadhihirisha maoni na mtazamo wa PK mwenyewe ambao haujathibitishwa na takwimu yoyote. Mshiriki huyu hajaeleza kama kauli yake imetokana na utafiti wowote. Mshiriki huyu basi amekiuka kanuni ya ukweli kwa kutoa kauli isiyoweza kuthibitika.

Kauli ya 157. HKK: Watu wa githu walifunga biashara zao ili wakuone vile wanakupenda enyewe unapendwa central.

HKK anakiuka kanuni ya ukweli kwa kutoa kauli isiyo ya kweli. HKK anadai kuwa watu wa Githurai walifunga bishara zao ili wamwone mhe. Odinga kwa sababu anapendwa sana mlima Kenya. Kauli hii si kweli kwa sababu wafanyabiashara katika eneo la Githurai walifunga biashara zao kwa hofu ya vurugu kuzuka. Hali hii inathibitishwa na taarifa ya habari katika gazeti la Taifa Leo la tarehe 28, Januari, 2021 inayoeleza kuwa biashara nyingi hazikufunguliwa kufuatia hofu ya vurugu kuzuka. Ithibati kutoka kwa gazeti hili inaifanya kauli ya HKK kuwa si kweli.

Kauli ya 204. WM: Si yenu madynasty Kenya yetu inapenda mahustlers kina mama mboga na pia mbogi ya bodaboda tusisahau madereva wote.

Mwitiko

JBJ: **WM,… madere si hustler kama nyinyi baba mbonga.**

Katika kauli hii, JBJ anakiuka kanuni ya ukweli kwa kukana kauli ya mzungumzaji moja kwa moja. JBJ anakataa kauli iliyotolewa na WM kwa kueleza kuwa madereva si hasla kama wao baba mboga. JBJ kukataa kauli ya WM kunadhihirisha kuwa hakuna ukweli wowote katika kauli iliyowasilishwa na WM. Mshiriki huyu ametumia mbinu ya kukana kauli ya mzungumzaji ili kukiuka kanuni ya ukweli.

242. NEL: Hii imefanya baba ametype Kiswahili kuna shida mahali…

Mwitiko

AAO: **ATA Mudavadi alisimama kama president na vice *president* wake hakumvotia.**

Katika mfano huu, AAO aliitikia kauli ya NEL kwa kutoa kauli isiyo na ukweli. AAO alidai kuwa aliyekuwa mgombea mwenza wa mhe. Mudavadi katika uchaguzi wa mwaka wa 2013 hakumpigia kura. Kauli hii inakiuka kanuni ya ukweli kwa sababu haiwezi kuthibitika licha ya kutokuwepo na ushahidi kuwa huyo mgombea mwenza hakumpigia kura. Isitoshe, kauli ya AAO inapingwa na taarifa ya habari katika gazeti la *Taifa Leo* la tarehe 10, Januari 2021 iliyomnukuu mhe. Kioni ambaye alikuwa mgombea mwenza wa mhe. Mudavadi akieleza ukweli wa kilichotokea. Mhe. Kioni alieleza kuwa kinyume na habari potovu zilizoenezwa, ukweli ni kuwa alimpigia mhe. Mudavadi kura wakati wa uchaguzi wa 2013. Kutokana na ithibati hii, ni dhahiri kuwa kauli ya AAO si kweli.

> Kauli ya 156. FF: Baba kusema tu ukweli hiyo kujumuika haijatoka kwa Kiswahili chako.
>
> Mwitiko
>
> 243. AK: **FF, Baba ni mwana siasa pekee kutoka nyanza anayejua Kiswahili sanifu**.

Katika kauli ya 156, FF anakiuka kanuni ya ukweli kwa kusema kuwa msamiati 'kujumuika' haukutokana na Kiswahili cha mhe. Odinga. Haya ni maoni yake mwenyewe ambayo yanaweza kupingwa na msikilizaji. FF hajatoa ithibati kuhusu dai lake hivyo kauli yake haina ushahidi wowote na unaaminiwa tu na mzungumzaji mwenyewe. Katika kauli ya 243, AK anatofautina na kauli iliyotolewa na FF kwa kueleza kuwa mhe. Odinga ndiye mwanasiasa wa pekee kutoka Nyanza anayejua Kiswahili sanifu. Kauli hii inakiuka kanuni ya ukweli kwa sababu kuna wanasiasa wengi kutoka Nyanza wanaokifahamu na kukielewa Kiswahili sanifu. Hivyo, haya ni maoni ya AK ambayo hayajathibitishwa na hayana ushahidi wowote.

> Kauli ya 91. AB: Kwani nani amesema hii Kenya ni ya wachache??

AB anakiuka kanuni ya ukweli kwa kukana kauli ya mzungumzaji moja kwa moja. Mshiriki huyu anatumia kipengele cha kukataa kauli ya mzungumzaji kuwa Kenya si ya wachache ili kukiuka kanuni ya ukweli. Kupitia kwa kipengele hiki, AB analenga kudhihirisha kuwa kauli iliyotolewa na mhe. Odinga haina ukweli wowote.

> Kauli ya 159. RRT: Asante baba tulifunga biashara tukuje tukusikie.

Kauli ya RRT inakiuka kanuni ya ukweli kwa sababu si kweli. RRT anaeleza kuwa walifunga biashara zao ili waje wamsikilize mhe. Odinga. Kauli hii si kweli kwa kuwa gazeti la *Taifa Leo* la tarehe Januari 28, 2021 linaeleza kuwa biashara katika eneo la Githurai zilifungwa kwa hofu ya kuzuka kwa vurugu. Ushahidi kutoka kwa gazeti hili unaifanya kauli ya RRT kuwa si kweli.

> Kauli ya 133. R: Tunajua tu mjaluo akiona watu wakirusha mawe anafurahia.

Kauli hii inadokeza maoni ya mshiriki R kuwa mjaluo huwa na furaha kila wakati akiona mawe yakirushwa. Kauli hii haijathibitishwa na utafiti wowote wala hakuna ushahidi wowote kuiunga mkono. Kanuni ya ukweli unamhitaji mzungumzaji kutoa kauli ambazo anauhakika nazo na ambazo zinaweza kuthibitika. Kwa kuwa ni maoni ya mshiriki, kauli hii inakiuka kanuni ya ukweli.

Kauli ya 94. IWW: Uongo nilikuwa hapo na sikuskia hiyo.

IWW anatumia kipengele cha kukana kauli ya mzungumzaji moja kwa moja ili kukiuka kanuni ya ukweli. Mshiriki huyu anakataa ujumbe uliowasilishwa na mhe. Odinga na kuueleza kama usio wa kweli. IWW anaeleza kuwa alikuwa katika eneo la Githurai na hakuweza kuyasikia yanayoelezwa na mhe. Odinga. Kukataa kauli ya mzungumzaji hukiuka kanuni ya ukweli.

Kauli ya 160. DE: Kumbe ni ukweli hakuna corona Kenya, nilikuwa napita tu..

Kauli hii inakiuka kanuni ya ukweli kwa kuwa si ya kweli. DE anaeleza kuwa kutokana na ziara ya mhe. Odinga kule Githurai, ni kweli hakuna corona nchini Kenya. Mshiriki huyu anatumia kejeli kuwasilisha hoja yake. Anakejeli kitendo cha mhe. Odinga kuandaa mkutano wa kisiasa wakati virusi vya corona vingali vinatatiza nchi. Mzungumzaji akitumia kauli yenye kejeli hukiuka kanuni ya ukweli. Isitoshe, kauli ya DE si kweli kwa kuwa taarifa iliyochapishwa katika gazeti la *Taifa Leo* la tarehe 27 Januari 2021, inadhihirisha kuwa maambukizi ya virusi vya corona viliendelea nchini. Katika tarehe hiyo, Kenya ilinakili visa vipya 130 vya corona. Taarifa hii inaifanya kauli iliyotolewa na DE kuwa si ya kweli hivyo inakiuka kanuni ya ukweli inayomtaka mzungumzaji kutoa kauli zilizo na ukweli.

Kauli ya 161. MM: Ndio Baba, hata kama kuna corona, lakini kwa mkutano wako corona huwa inatoroka, tatizo ukishamaliza na ukienda corona huwa inarudi mahali pake.

Katika kauli hii, MM anatumia kipengele cha kejeli kukiuka kanuni ya ukweli. Mshiriki huyu anakejeli kitendo cha mhe. Odinga kuandaa mikutano ya kisiasa katika eneo la Githurai licha ya kuwepo kwa virusi vya corona nchini. Katika kumkejeli, MM anaeleza kuwa katika mkutano wake virusi vya corona hutoroka lakini vinarudi punde tu akishamaliza. Mzungumzaji hukiuka kanuni ya ukweli anapotoa kauli inayomkejeli msikilizaji wake.

Kauli ya 162. JM: Baba anaogopwa hata na corona, yeye n coronaproof

JM anamkejeli mhe. Odinga kwa kuandaa mkutano wa kisiasa licha ya kuwepo kwa virusi vya corona nchini. katika kumkejeli, JM anaeleza kuwa mhe. Odinga anaogopwa na virusi hivyo. Mshiriki huyu ametumia kipengele cha kejeli ili kukiuka kanuni ya ukweli.

Kauli ya 103. FT: Githurai ni Ruto.

Katika mfano huu, FT anaeleza kuwa eneo la Githurai ni ngome ya kisiasa ya mhe. Ruto. Kauli yake haijatokana na utafiti wowote hivyo haiwezi kuthibitishwa. Kauli hii basi inadhihirisha maoni ya mshiriki huyu ambayo yanaweza kupingwa na washiriki wengine. Hali ya mzungumzaji kutoa kauli isiyoweza kuthibitika na asiyo na ushahidi wa kutosha hukiuka kanuni ya ukweli.

Sasisho ya 2

> Kauli ya 13. SR: Ni sawa Baba hii ndio kitu ya kwanza umeshinda tangu uzaliwe.

SR anaeleza kuwa kupita kwa mswada wa BBI ndiko kitu cha kwanza ambacho mhe. Odinga amewahi kushinda tangu azaliwe. Kauli hii si kweli kwa kuwa gazeti la '*The Standard*' la tarehe 23 Julai 2012 linadhihirisha namna mhe. Odinga alikuwa mbunge wa Langata kwa muda mrefu kuanzia mwaka wa 1992 hadi 2013. Ushahidi uliopo katika gazeti hili basi unapinga kauli iliyotolewa na SR, hivyo kuifanya kuwa si ya kweli.

> Kauli ya 98. RK: Waaa Baba kuliko kutuletea BBI si wewe ndio ungejiodoa kwa wagombeaji juu wewe ndiye uleta vita juu ya uchaguzi huku ukipeleka makesi kortini na kuboycot vitu za makampuni zenye unachukia…

RK anatoa kauli kuwa mhe. Odinga ndiye huleta vita vinavyotokea nchini kila baada ya uchaguzi. Kauli ya RK haijatokana na utafiti wowote ila inaonyesha maoni yake kuhusu kinachosababisha vita vya baada ya uchaguzi. RK basi anakiuka kanuni ya ukweli kwa kudai kuwa mhe. Odinga ndiye husababisha vita hivyo. Kauli yake haina thibitisho lolote.

> Kauli ya 128. JM: Ruto hawezani na baba, ata akizaliwa baba alikuwa tu kua siasa.

JM anakiuka kanuni ya ukweli kwa kueleza kuwa mhe. Ruto hawezani na mhe. Odinga kisiasa mbali na kuwa hata mhe. Ruto akizaliwa, mhe. Odinga tayari alikuwa katika siasa. Kauli kuwa mhe. Ruto hawezani na mhe. Odinga hudhihirisha maoni ya JM mwenyewe ambayo hayana ithibati yoyote. Pia, si kweli kuwa wakati mhe. Ruto alikuwa akizaliwa mhe. Odinga tayari alikuwa katika siasa. Hii ni kwa sababu ushahidi kutoka kwa shiriki la habari la *DW* unaonyesha kuwa mhe. Odinga alijitosa katika ulingo wa siasa nchini Kenya mwaka wa 1992 alipochaguliwa kuwa mbunge wa Langata. Kwa hivyo, si kweli kusema kuwa mhe. Odinga alianza siasa wakati mhe. Ruto akizaliwa kwa sababu ushahidi kutoka kwa Wikipedia unaonyesha kuwa mhe. Ruto alizaliwa mwaka wa 1966, hata kabla mhe. Odinga ajitose siasani.

> Kauli ya 97. SM: Hakuna bbi ilipita walipisha magari.

SM anakiuka kanuni ya ukweli kwa kueleza kuwa mswada wa BBI haukupitishwa na madiwani ila walipitisha magari. Kauli ya SM si kweli kwa sababu madiwani walipiga kura ili wapitishe mswada huo. Hali hii inaungwa mkono na gazeti la *Taifa Leo* la tarehe 24 Februari 2021 linaloeleza

namna mabunge ya kaunti yalipitisha mswada wa marekebisho ya katiba kupitia mapendekezo ya ripoti ya mpango wa maridhiano (BBI).

> 244. PBW: MCA mtajua sio wananchi.

Katika kauli hii, PBW ankiuka kanuni ya ukweli kwa kutoa kauli ambayo si kweli. Anaeleza kuwa madiwani katika mabunge ya kaunti si wananchi. Huu ni uwongo kwa sababu madiwani hao ni wananchi kwanza kabla ya kuwa madiwani. Udiwani umetokana na uwananchi wao ndiposa walichaguliwa kuwa madiwani. Kauli hii basi si kweli.

> Kauli ya 50. JD: Hakuna mwanaume mwizi kama raila. Huwa uko na sura mbaya na bado unaibia Kenyans. Constitution na bbi zimesaidia nani ka si nyinyi pekee. Sina ubaya nikikuita jambazi.

JD anawasilisha maoni yake kuwa hakuna mwizi kama mhe. Raila. Kauli hii inadhihirisha maoni ya mzungumzaji ambayo hayajathibitishwa. Kauli hii basi inakiuka kanuni ya ukweli kwa sababu mzungumzaji ametoa kauli ambayo haijatokana na ushahidi wowote.
<u>Sasisho ya 3</u>

> Kauli ya 55. EE: Aliiba pesa ya corona na vinyangarika wake. Alidhani anaeza hepa.

EE anaeleza kuwa mhe. Odinga pamoja na wenzake waliiba pesa zilizotengewa virusi vya corona. Haya ni maoni ya EE ambayo hayajathibitishwa na yanaweza kupingwa na washiriki wengine. Kauli hii basi inakiuka kanuni ya ukweli kwa kuwa haijengwi kwa ushahidi wowote.
<u>Sasisho ya 5</u>

> 245. JMN: Mungu mkumbuke baba Kenya imesimama bila baba.

Kauli hii inakiuka kanuni ya ukweli kwa kudhihirisha kauli isiyo ya kweli. JMN anaeleza kuwa Kenya imesimama kwa sababu mhe. Odinga ni mgonjwa. Kauli hii si kweli kwa sababu kila shughuli nchini ilikuwa ikitekelezwa na wanaohusika. Lengo la JMN kutoa kauli hii isiyo ya kweli ni kuonyesha umuhimu wa mhe. Odinga nchini.

**6.4 Ukiukaji wa Kanuni ya Namna**

Kanuni hii hukiukwa mzungumzaji anapokosa kusema au kujibu swali kwa njia inayoeleweka kwa urahisi. Katika kanuni hii, mzungumzaji anahitajika kuepukana na utata anapozungumzia habari fulani na awe na mpangilio katika mazungumzo yake. Mzungumzaji anafaa kutoa habari zake kwa namna inayoeleweka vizuri na kwa njia wazi. Kulingana na Grice (1975), kanuni ya namna hukiukwa ikiwa mzungumzaji atatumia kauli tata, ikiwa atatia chumvi kauli zake au ikiwa mzungumzaji atatumia misimbo isiyoeleweka kwa msikilizaji wake. Katika diskosi ya siasa, hali hii ilidhihirika zaidi kupitia matumizi ya misimbo na matumizi ya kauli ambazo zinamlazimu msikilizaji kutumia umaanisho ili kupata maana. Kupitia vipengele hivi, mtafiti

aliweza kukusanya kauli zifuatazo ambazo zilikiuka kanuni hii.

Sasisho ya 1

> Kauli ya 205. ER: Youths huwa hamuangalii maisha yenu na familia zenu before mfanye kitu mbaya, imagine unalipwa kuharibu sura na jina la mtu yet hujui kuna wale wanakuhitaji sana kuliko aliyekupa doo…acheni na siasa coz utarudi kula kwako mboga wao upande mwingine wakila michuzi Tena kwa meza moja.
>
> Mwitiko
>
> DW: **Baba ata asiponilipa, lazima nifanye vile anataka…heri nife bora baba awe prezo.**

Mwitiko uliotolewa na DW unakiuka kanuni ya namna kwa kuwa unahusisha matumizi ya chuku. DW ameitikia kauli iliyotolewa na ER kwa kueleza kuwa hata mhe. Odinga asipomlipa, yeye lazima angeendelea kufanya anavyotaka mhe. Odinga. Hata hivyo, DW anatia chumvi kauli yake kwa kueleza kuwa ako tayari kufa mradi mhe. Odinga awe rais. Kupitia kauli hii, DW anadhihirisha tu kiwango cha ufuasi wake kwa mhe. Odinga. Kutokana na chuku hii, kanuni ya namna imekiukwa na mzungumzaji.

> Kauli ya 225. JO: Sawa baba, but nasikia ety oh mara ohh, ni ukweli?

Kauli hii inakiuka kanuni ya namna kwa kuwa ni tata hivyo ujumbe wake si dhahiri. JO anaeleza mhe. Odinga kuwa amesikia ety oh mara ohh, ujumbe ambao haueleweki. Kauli hii basi humtatiza msikilizaji katika kufasiri maana yake kwa kuwa ni tata. Matumizi ya kauli tata hukiuka kanuni ya namna.

> Kauli ya 37. SM: Baba utapata kura zote Central Kenya, saidia rais Kenyatta kufagia hawa wezi wanaiba billion bili kila siku.

SM alimhakikishia mhe. Odinga kuwa angepata kura zote zilizomo mlima Kenya. Kauli hii imejaa chuku kwa kuwa hakuna uwezekano wa mhe. Odinga kuzoa kura zote katika eneo hilo kutokana na wimbi la kisiasa katika eneo hilo ambalo halivumi kuelekea upande wake. Pia, kuwepo kwa waniaji wengine kunafanya hali hii kuwa ngumu. SM basi alitia chumvi kauli yake ili kudhihirisha kuwa mhe. Odinga anauungwaji mkubwa katika mlima Kenya. Kauli hii basi inakiuka kanuni ya namna.

Sasisho ya 2

> Kauli ya 186. SM: Uzuri debe tutaiangusha…
>
> Mwitiko
>
> KJR: SM, hiyo debe inahesabiwa na serikali bado sio **wanjiku**.

Katika kauli hii KJR anatumia msimbo 'wanjiku' kukiuka kanuni ya namna. KJR anaeleza kuwa kura inahesabiwa na serikali wala si wanjiku. Matumizi ya msimbo 'wanjiku' yanamfanya

msikilizaji wa kauli hii kutoelewa maana yake kwa sababu umetumiwa kumaanisha maana tofauti na jina la kawaida la mhusika fulani.

Kauli ya 12. DK: Wee wacha chocha!

Kauli hii inakiuka kanuni ya namna kwa kuwa inahusisha matumizi ya msimbo ambao maana yake huenda msikilizaji haelewi. DK antumia msimbo 'chocha' kukiuka kanuni ya namna. Maana ya msimbo 'chocha' ni tata hivyo msikilizaji atatizika kuelewa maana yake.

246. SV: Mzae wacha uwaganis, utalia tena ukisema nusu mkeka, kwa ground ni kuzing, design ya ombitho, ilete tuipige kuni, si ndo tuko na kura.

Kauli hii inakiuka kanuni ya namna kwa kuwa inahusisha matumizi ya misimbo mbalimbali ambayo maana yake msikilizaji atatatizika kuelewa. SV anatumia misimbo yenye maana tata 'uwaganis', 'nusu mkeka', 'kuzing', 'ombitho' na 'tupige kuni'. Maana za misimbo hii si wazi hivyo msikilizaji hataelewa ujumbe uliowasilishwa kikamilifu.

Kauli ya 20. OAO: Sasa ilete kwa mbogi tuiangushe.

Katika kauli hii mshiriki OAO anatumia msimbo 'mbogi' kukiuka kanuni ya namna. Maana ya msimbo huu si dhahiri hivyo msikilizaji wa ujumbe wa kauli hii atatizika kuuelewa. Matumizi ya msimbo hukiuka kanuni ya namna.

247. Tanks Baba, tuko pamoja na tutakufa pamoja.

Kauli hii inakiuka kanuni ya namna kwa kutia chumvi kauli ya mzungumzaji. Mshiriki huyu anamweleza mhe. Odinga kuwa wangekufa pamoja naye. Hii ni kauli tata ambayo maana yake si dhahiri kwa msikilizaji kwani inadokeza maana zaidi ya moja. Pia, mshiriki huyu amepiga chuku ufuasi wake kwa mhe. Odinga kiasi cha kuwa tayari kufa naye. Hii ni mbinu ya chuku ambayo hukiuka kanuni ya namna.

Kauli ya 47. DN: Baba 4 Mashamba 0. Round hii GG imekataa.

Kauli hii imehusisha misimbo ambayo maana zao si dhahiri kwa msikilizaji. Msimbo 'GG' haudhihiriki kimaana hivyo kutatiza kimaana. Msimbo huu hukiuka kanuni ya namna.

Kauli ya 228. JMW: Leo utalala na viatu.

Maana katika kauli hii ni tata kwa sababu kauli hii inawasilisha zaidi ya maana moja. Msikilizaji wa kauli hii basi atatatizika kung'amua ni maana gani aliyolenga kuwasilisha mzungumzaji wake. Kauli hii basi ni tata hivyo kukiuka kanuni ya namna.

Kauli ya 229. OVA: Baba siwezi lala leo.

Katika kauli hii, OVA ametia chumvi hisia zake baada ya mswada wa BBI kupitishwa na mabunge ya kaunti. Kulingana naye, hangeweza kulala siku hiyo huenda kutokana na furaha alizonazo. Kanuni hii imepiga chuku hisia za mzungumzaji hali ambayo inakiuka kanuni ya namna.

Sasisho ya 3

248. ZC: Baba pona haraka ndiyo nikule..

ZC ametumia mbinu ya chuku kukiuka kanuni ya namna. Kulingana naye hali kwa sababu mhe. Odinga ni mgonjwa. Mshiriki huyu ametia chumvi kauli yake ili kudhihirisha namna angependa mhe. Odinga apone.

Kauli ya 245 JMN: Mungu mkumbuke baba Kenya imesimama bila baba.

Kauli hii inakiuka kanuni ya namna kwa kuwa inahusisha mbinu ya chuku. JMN anamwomba Mungu amponye mhe. Odinga kwa sababu Kenya haisongi bila yeye. JMN amekiuka kanuni ya namna kwa kudokeza Kenya imesimama bila mhe. Odinga hali ambayo si kweli.

Sasisho ya 5

Kauli ya 174. ZL: Zabloan amemea kumea.

Katika mfano huu, ZL ametumia msimbo 'zabloan' kukiuka kanuni ya namna. Msimbo huu hudhihirisha maana zaidi ya moja kwa msikilizaji. Maana tata katika msimbo huu humfanya msikilizaji kupata ugumu katika kufasiri mana kamili iliyolengwa na mzungumzaji.

**7.0 Hitimisho**

Utafiti uliweza kubainisha kuwa washiriki wa mtandao wa *Facebook* hukiuka kanuni zote za ushirikiano wanapojadili maswala ya kisiasa nchini. Washiriki wa mtandao wa *Facebook* hukiuka kanuni ya kiasi, kanuni ya uhusiano, kanuni ya namna na kanuni ya ukweli. Utafiti ulibainisha kuwa kanuni ya kiasi hukiukwa sana na washiriki wa mtandao wa *Facebook* wanapojadili masula ya kisiasa nchini. Kanuni ya kiasi ilijitokeza kwa asilimia 32.9 huku kanuni ya namna ikikiukwa kwa asilimia 16.5. Katika kuchunguza kanuni za ushirikiano zinazokiukwa na washiriki wa mtandao wa *Facebook*, mtafiti alibainisha kuwa ukiukaji wa kanuni za ushirikiano hutokana na sababu mbalimbali. Kwanza, ukiukaji huu hutokana na kuwepo kwa washiriki wengi ambao hutumia mtandao wa *Facebook*. Hali hii huwapa washiriki hao nafasi ya kutozingatia kanuni hizo kwani hawajali jinsi wasikilizaji wao watapokea jumbe zao. Pia, mgongano wa kanuni za ushirikiano husababisha kanuni za ushirikiano kukiukwa na washiriki wa mtandao wa *Facebook*. Kutokana na mgongano huu, mzungumzaji hujipata katika hali ya kukiuka kanuni fulani ili kuzingatia vipengele vya kanuni nyingine. Kwa mfano, katika utafiti huu, kauli ya 231 inakiuka kanuni ya kiasi ili kuhifadhi kanuni ya ukweli. Isitoshe, utafiti ulibainisha kuwa washiriki wa mtandao wa *Facebook* hukiuka kanuni za ushirikiano ili kuficha siri kutoka kwa wasikilizaji wao au ili wajiepushe na kutoa habari muhimu kwa wasikilizaji wao. Hata hivyo, licha ya ukiukaji huu, mawasiliano huendelea bila tatizo lolote.

**8.0 Mapendekezo**

Mtafiti anapendekeza tafiti zifanywe kuhusu ukiukaji wa kanuni za ushirikiano katika mitandao mingine kama vile *Twitter* na *Instagram*. Pia, utafiti uweze kufanywa kuhusu sababu za ukiukaji wa kanuni hizi katika mitandao ya kijamii.

**Funding**: This research did not receive any form of funding.

**Disclaimer Statement**: This work is part of a thesis submitted to Kisii University for award of Masters Degree in Kiswahili.

**Author bionate**: Akello Odiaga Walter is a student at Kisii University persuing Masters Degree in Kiswahili in the department of Languages, Linguistics and Literature. He's a trained teacher of Kiswahili from Kenyatta University. Akello has a lot of interest in politeness in communication.

**Authorship and level of contribution**: My supervisors, Dr. Riro Matinde and Dr. Oluoch Stephen, were quite handy in helping me come up with this document. They tirelessly guided me in every step I took in writing this research.

**Marejeleo**

Abdul Wahid et al (2000). 'Conversational Maxims and Implicature: Evidence from Arabic for Quantity and Relation'.Unpublished Ph.D. Thesis, University of Basra

Arezou (2014). 'The Violation of Cooperative Principles and Four Maxims in Iranian Psychological Consultation'. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa, Chuo kikuu cha Otago

Arthanti N. (2013). 'Violation of Grice's Maxims in the Gartified 'Hangs Out' Comic: Comparison between Source Text (ST) and Target Text (TT)'. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa, Dian Nuswanton University Semarang.

Ayunon C. (2018). Gricean Maxims Revisited in FB Conversational Posts. Its Pedagogical Implications. *TESOL International Journal, v13 n4 p82-95 2018.*

Badejo B. (2006). *Raila Odinga*: An Enigma in Kenyan Politics. Nairobi, Yintab Books

Barasa N. (2014). Discursive strategies in Kenya's 2008 post election consultation discourse. Phd Thesis, Laikipia University.

Boshier, R (1990). Socio- Psychological factors in Electronic Networking. *Internal Journal of Lifelong Education, 9(1), 49-64.* Retrieved on March 8, 2021 from https: www.learntechlib.org/p/142582/.

Bousfield, D. (2008). *Impoliteness in Interaction*. Amsterdam: John Benjamin Publishing Company.

Creswell J. (2013). *Qualitative Inquiry and Research design*. London. SAGE Publications Inc.

Davies, B. L. (2007). Grice's Cooperative Principle: Meaning and Rationality. *Journal of Pragmatics, 39(12), 2308-2331.*

Dewanata P. (2018). 'The Analysis of Grice's Cooperative Principle on the Responses of Indonesian Politicians: Pragmatic Study'. Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa, Mataram University.

Dwyer et al (2007). Trust and Privacy concerns within Social Networking Sites: *Acomparison of Facebook and Mypace', AMCIS 2007 proceedings 339. https.//aisle.aisnet.org/amcis2007/339*

Enon, C. J. (1998). *Education Research and Measurement*. Department of Distance Education: Makerere University; Uganda.

Gay, L. & Diehl, P. (1992) *Research Methods for Busines and Management*. New York: Mcmillan

Goldstein J. and Rotich, J(2008). Digitally Networked Technology in Kenya's 2007-2008 Post Election Crisis. Retrieved from: https//cyber.law.harvard.edu/sites/cyber.law.harvard.edu/files/Goldstein&Rotich_Digitally_Networked_Technology_Kenyas_Crisis.pdf.pdf

Grice, H.P. (1975). "Logic and Conversation."*In Peter Cole & Jerry Morgan (eds.) Syntax and Semantics, Volume 3: Speech Acts, pp. 41–58*. New York, NY: Academic Press

Herring, S. (2001). *The Handbook of Discourse Analysis*. Oxford: Blackwell

Hiltz, R and Turoff, M (1993). *The Network Nations*. Human communication via computer (Rev.ed). Cambridge: MIT Press.

Holloway V. and Wheeler S. (2002). *Qualitative research in nursing*. 2nd edition. Oxford. Blackwell Publishing

Junaedi D.(2017). 'The Violation of Cooperative Principles through Gender Language Features in '*Love, Rosie' Film'*. Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa , Alauddin State Islamic University of Makassar.

Kiesler, S et al (1984). Social Psychological aspects of Computer-Mediated Communication. *American Psychologist, 39 (10), 1123-34.*

Kim, M and Raja, S (1991). Verbal Aggression and Self- discussions on Computer bulletin boards. *Paper presented at the Annual Meeting of the International Communication Association (41st ) Chicago, 12 May 23-27,1991. (ERIC Document Reproduction No. ED 334-620).*

Leech, G.(1980) *Explorations in Semantics and Pragmatics*. Amsterdam: John Benjamins.

Levinson, C. (1983) *Pragmatics*. Cambridge: Cambridge University Press.

Locher, M. A. (2010). Introduction*:* Politeness and Impoliteness in Computer-mediated Communication. *Journal of Politeness Research, 6, 1-5*

Luvega D. & Obara V. (2021, Januari, 10). Kioni Asutwa kwa Madai Hakumpigia kura Mudavadi Alipokuwa mgombea mwenza. *Taifa Leo*. Retrieved from www. taifaleo.nation.co.ke

Mugenda,O. & Mugenda, A. (2005). *Research Methods*: Quantitative Approaches. Nairobi: ACTS Press.

Ndavula J. (2013). Social Media Adoption as Alternative Platform for Political Marketing in Kenya. *African Multidisciplinary journal of research, ISSN: 2518-2986(online) 1(1), 26-411-2016*

Nduva, M (2016). Media portrayal of women leaders in Kenya: *An intersection of female politicians and newspaper narratives*. Unpublished thesis, University of Nairobi.

Ochieng J. & Wasonga C. (2021, Januari, 28). Vijana Wavurugu Mkutano wa Kupigia Debe BBI Alioongoza Raila. *Taifa Leo*. Retrieved from www. taifaleo.nation.co.ke

Putra I. (2014). The Grice's Cooperative Principles in Transcript of Beyonce Interview on *Piers Morgan Tonight*. Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa, State Islamic University Syrif Hideyatullah

Smolensky,M et al. (1990). The Influence of Task Type, Group Structure and Extraversion on Uninhibited Speech in Computer-Mediated Communication. *Computers in Human Behavior, 6(3), 261-272.*

Waki Report (2008). Commission of Inquiry into Post Election Violence. Nairobi. http://www.google.com

Wasonga C. (2021, Februari, 24). Raila Achangamkia Kupitishwa kw BBI. *Taifa Leo.* Retrieved from www. taifaleo.nation.co.ke

Wasonga C. (2021, Januari, 27). *COVID 19*: Mmoja Afariki, Serikali Yathibitisha Visa Vipya. *Taifa Leo*. Retrieved from www. taifaleo.nation.co.ke

Westling, M (2007). Expanding the Public Sphere: *The Impact of Facebook on Political communication (pp. 1-13)*

Yule, G. (1996) *Pragmatics*. London: Oxford University Press.